




**WABAINI** madini yanachimbwa hifadhi ya msitu

UKURASA 17




UKURASA 11

Jumatatu Agosti 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581409

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/th...

## DINI NA SIASA

# Kikwete aonya vikali



Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete

**ASEMA** nchi itakuwa pabaya; waraka mwingine watolewa... *Endelea Ukurasa wa 2*

UKURASA WA 4

## WAZIRI AELEKEZA KUREKEBISHWA MADIRISHA YA SHULE

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, amemtaka fundi aliyepewa kandarasi ya kujenga Shule mpya ya Msingi ya Kona Nne, Halmashauri ya Wilaya Ushetu, mkoani Shinyanga, kurekebisha...

UKURASA WA 5

## VIFAA KUKABILI TEMBO VYAPELEKWA NACHINGWEA



SERIKALI imepeleka vitendea kazi kwa ajili ya kufukuza tembo wanaovamia makazi ya watu ikiwa ni kujibu kero ya muda mrefu ya wakazi wa kata za wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, wanaosumbuliwa na wanyama hao.

Vitendea kazi hivyo ni ndege aina...



Rais Samia Suluhu Hassan akikabidhi tuzo ya utendaji bora katika Sekta ya Fedha kwa mwaka unaoishia Juni 2023 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa NIC Insurance, Dk. Elirehema Doriye (wa pili kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya NIC, Justine Mwandu (kulia), kwenye ufunguzi wa mkutano wa wakuu wa taasisi na wenyeviti wa bodi kwa sekta za umma jijini Arusha juzi. Wengine ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kushoto ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uwekezaji na Mipango, Prof. Kitila Mkumbo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Biteko: Tanzania, India zina uhusiano kiuchumi

UKURASA 3

# Wadau wachambua mitaala mipya elimumsingi, vyuo ualimu

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA YAANZA MAUAJI CAF, AZAM YADUNDWA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, wakifakamia nyama na ndizi za kuchoma zilizokuwa zikiuzwa bila kuchukua tahadhari za kiafya katika eneo la Temeke, hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JK aonya vikali kuchanganya dini na siasa

**Na Waandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete amewataka Watanzania kuwanyanyapaa baadhi ya viongozi wa dini, wanaochanganya dini na siasa ikiwa ni pamoja na kuwalazimisha waumini wao kuamini mrengo wa siasa wanazoziamini.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo jana wilayani Butiama, mkoani Mara alipohutubia waumini wa Kanisa la Wadventista Wasabato wakati wa uwekaji wa Jiwe la Msingi na kukabidhi jengo la Kanisa la Chalia wilayani humo.

Alisema kati ya tunu muhimu za kulinda amani ya Watanzania ni pamoja na kutokuchanganya dini na masuala ya kisiasa na kusisitiza endapo tunu hiyo itavunjwa, "nchi imekwisha", hivyo kuwataka Watanzania kuwanyanyapaa na kutokuwasikiliza viongozi wanaochanganya masuala hayo kwa maslahi yao binafsi.

"Kama kuna viongozi wa dini wanaotaka kutuelekeza kuitumia dini kwa manufaa ya kisiasa na viongozi wa kisiasa, wanaotaka kuitumie dini kwa manufaa yao ya kisiasa, ninawaombeni ndugu zangu tuwanyanyapae,"alisema Dk. Kikwete ambaye alikuwa Rais wa Tanzania tangu mwaka 2005 hadi 2015.

Aliendelea kusema kuwa siku ikifika ambapo wanachama wa chama cha siasa wakiuhusisha uumini wao na chama chao, huo utakuwa ndio mwisho wa nchi kwa kuwa vitakuwapo vyama vya siasa vya wakristo, waislamu pamoja na madhehebu mengine na hivyo kuhatarisha hali ya amani ya nchi.

Alisema; "Kuwafanya Watanzania kuyatazama masuala ya kisiasa, kiserikali pamoja na utawala kwa mtazamo wa dini zetu, ni jambo hatari. Vilevile, watu kuyatazama masuala ya dini kwa mtazamo wa siasa za vyama vyao, sio jambo lenye afya kwa taifa letu."

Kwa mujibu wa Kikwete, yote mawili kwa pamoja yataathiri umoja, mshikamano usalama na utulivu uliopo nchini kwa sasa, huku akitolea mfano wa kilichotokea Zanzibar wakati wa uongozi wake.

Alikumbusha kuwa kipindi hicho baadhi ya waamini wa Kiislamu walitengana na kugawana misikiti kwa kile alichokiita kutofautiana katika itikadi za kisiasa.

"Hili jambo lilitugharimu sana mpaka kuimarisha hali ya visiwani humo kuweka Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hali ambayo tusingependa ijirudie tena, siyo kwa visiwani (Tanzania Zanzibar) wala (Tanzania) Bara," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Kikwete alizipongeza taasisi mbalimbali za dini katika kuhakikisha wanaimarisha huduma mbalimbali za kijamii, zikiwamo za afya, elimu, maji na miundombinu.

**WARAKA MWINGINE**

Jana, Mkurugenzi Mkuu Idara ya Ulinzi na Itifaki wa Baraza la Mitume na Manabii Tanzania (BACCT), Dk. Peter Abubakari, alitoa tamko la kuwataka wakosoaji wa suala la uwekezaji bandarini kufanya hivyo kwa maneno yenye staha na kuheshimu mamlaka.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, baraza hilo lilieleza mambo saba ya kuzingatia kuhusu ukosoaji huku likimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na Watanzania wote bila kubagua.

Pia lilimpongeza kwa kushiriki shughuli za Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na chama chake (CCM), kushiriki shughuli za makanisa na misikiti kwa upendo mkubwa na kutaja msimamo wao kuhusu sakata hilo.

Baraza hilo liliorodhesha mambo hayo saba ambayo ni; "Mawazo ya Kanisa Katoliki ifahamike kuwa siyo mawazo ya Watanzania wote, mkataba mmoja tu wa bandari haupaswi kutumika kuvunja na kuivuruga amani ya nchi yetu.

"Udhalilishaji dhidi ya Rais, haukubaliki. Akosolewe kwa staha, serikali haiwezi kupokea mashinikizo ya madhehebu kuhusu kuendesha, yapo mengi sana atamsikiliza nani amwache nani?

"Viongozi wa dini tuna fursa ya kushauri tuitumie vizuri baada ya kushinikiza mambo. Sisi mitume na manabii tunakuunga mkono, tunaunga jitihada zako za kuleta maendeleo, uhuru wa kujieleza ingawa unatumika vibaya pamoja na kukuombea afya njema uendelee kushiriki katika matukio ya Watanzania wote bila kubagua imani za dini na itikadi za kisiasa."

**WARAKA KANISANI**

Jana katika makanisa mengi ya Kanisa Katoliki, Waraka wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), kuhusu uwekezaji bandarini ulisomwa na mapadri walioongoza ibada.

Wakizungumza na waandishi wa habari, waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Moyo Mtakatifu wa Yesu Jimbo la Singida, walisema waraka huo haumlengi mtu bali maslahi ya nchi na mali za nchi.

"Hakuna tamko linalomlenga mtu yeye kama yeye, bali linalenga maslahi ya nchi na mali za nchi na kwa kweli, hakuna mwenye nia yoyote mbaya," alisema Padri Samoni Gwanoga baada ya tamko hilo kusikilizwa na waumini kupitia sauti iliyorekodiwa ya mtangazaji wa Radio Vatican News.

Alisema nakala ya tamko hilo itagawiwa kwa kila jumuiya na vigango vyote vya ndani na nje ya mji, ili lisomwe na waumini wa Kanisa Katoliki waweze kujua kwa upana.

"Kama hujiamini, hujui, usitowe maelezo ya kupotosha, baki kwenye tamko na bahati mbaya siyo wote tunaoweza kulisoma na kulipa tafsiri nzuri, lakini kwa kuwa sio suala la kisiasa, ni suala la kanisani, ninaamini litatujengea umoja, upendo na mshikamano kama Watanzania kwa sababu hatima yetu sote ni moja - kujenga nchi yetu kwa upendo, umoja na mshikamano na kwa ushirikiano," alisema.

# Msechu aeleza puto lilivyosaidia kupungua kilo 17 miezi minane

**Na Halfani Chusi**

BAADA ya miezi minane tangu alipowekwa puto tumboni ili kupunguza uzito, Msanii wa Bongo Fleva, Peter Msechu, ameeleza maendeleo ya afya yake, akibainisha amefanikiwa kupunguza uzito kwa kilo 17.

Akihojiwa na chombo kimoja mtandaoni mwishoni mwa wiki, msanii huyo alisema amehangaika kwa muda mrefu kupunguza uzito ikiwamo kutumia mitishamba ya aina mbalimbali bila mafanikio, lakini tangu amewekwe puto, anahisi mwili umekuwa mwepesi na anaweza kufunga kamba za viatu.

Msechu alisema aliamua kufuata huduma hiyo kwa kuwa kwa muda mrefu alikuwa anahitaji kupunguza uzito lakini alikuwa anashindwa kujizuia kula chakula kizuri ikiwamo wali maharage, chakula anachopendelea zaidi.

"Kwa miaka mingi sana, nimekuwa nikihangaika kupungua, changamoto iliyokuwa inanigharimu ni kushindwa kujizuia kula chakula kizuri, ilikuwa mtihani mkubwa sana.

"Mimi sijawahi kushiba, nilikuwa sijui hisia ya kushiba ipoje, mpaka mama yangu alikuwa ananishangaa, ilikuwa wakipakua chakula ni labda kiishe au wanipokonye sahani," alisema Msechu anayejitambulisha kama Rais wa Wameza Maputo Tanzania.

Alisimulia kwamba uzito wake ulizidi kwa kuwa alishindwa kufanya mazoezi na kujizuia kula hasa pale alipoanza kushika fedha zake binafsi na kula anachokitaka. Akawa mnene kupindukia.

Msechu ambaye alikuwa na kilo 140 kabla ya kuanza kutumia huduma hiyo, alisema alipambana kwa muda mrefu kupunguza unene, akikumbusha alishawahi kufanya mazoezi na kupunguza kula, lakini juhudi hizo hazikuzaa matunda.

"Nilikuwa nikikutana na wali maharage, nilikuwa siwezi (kujizuia), lazima nile! Kwa sababu ndio chakula ninachokipenda sana, hata mke wangu akinizuia ninaamka hata usiku nakula.

"Kwa hiyo, nilipokuja kufanya utafiti, nikagundua kuwa puto linapunguza idadi ya chakula na hamu ya kula, kwa sababu awali nilikuwa ninaweza kula wali maharage kilo moja peke yangu, lakini tangu niliposwekewa puto, ninakula vijiko vitatu tu, kwangu hii ni tiba nzuri sana inanisaidia.

"Nilifanya utafiti hata kabla huduma hiyo haijaja nchini, nikashindwa gharama, nilitaka kwenda nchi za nje kama Uturuki nikaambiwa gharama yake Sh. milioni 35, Marekani nikaambiwa Sh. milioni 50, ilikuwa ngumu kwa sababu ya kipato nisingeweza kulipa hiyo fedha sasa ilivyokuja hapa nikasema hapahapa ndio pakuweka," alisema Msechu.

Alisema mwanzoni alikuwa anaogopa kutokana na maneno ya watu, lakini alipoona kuna watu wawili wameenda na wamepatiwa huduma hiyo na yeye akaamua kwenda, jambo analodai hajutii kufanya uamuzi huo.

"Nikaweka puto, ilikuwa Januari 26 mwaka huu, linaisha muda wake kwa mwaka mmoja lakini ndani ya miezi sita nilipungua kilo 17, japokuwa ndani ya miezi hiyo unaruhusiwa kuangalia kama unaona uzito umepungua unaweza kulitoa, ikiwa bado unaongezwa maji ili uendelee kupungua mpaka mwaka mmoja utakapokamilika," alisema.

Alikumbushia kuwa wakati ameanza kutumia huduma hiyo, hakufanya mazoezi ndani ya miezi mitano, jambo lililosababisha mwili wake kuchelewa kupungua na kuzua gumzo mitandaoni kwamba puto halifanyia kazi.

"Unapokuwa kwenye huduma hiyo, unatakiwa kufanya mazoezi, lakini kuna kosa nililifanya. Unapowekewa puto, inabidi ufanye mazoezi, ili ulisaidie liweze kufanya kazi vizuri. Kwahiyo, mwanzoni kama miezi mitano hivi sikufanya mazoezi, nikawa sipungui, niliwaza nitawaeleza nini watu na madaktari kule Mloganzila.

"Bahati nzuri nilikuwa tayari nimepungua kilo 17, nilipokwenda 'kucheki' wakanishauri nisilitoe mpaka mwezi wa 12 wakaliongeza maji kabla nilikuwa na kilo 140, lengo langu mpaka mwezi wa 12 nifike kilo 100 au 90," alisema.

Aliongeza: "Uzuri wa puto sio dawa kwamba unaandikiwa na daktari, unaridhia mwenyewe kuweka, sasa utaona utofauti kwa Tanzania ni Sh. milioni nne na nusu, nje ya ni zaidi ya Sh. milioni 15," alisema.

# Wadau watoa ushauri kuanza mitaala mipya

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa elimu nchini wamepongeza serikali kwa kuandaa rasimu ya mitaala mipya kwa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kuwa itakwenda kuleta mapinduzi ya elimu nchini na kuzalisha wataalamu wabobevu wa kutosha kutoka kada mbalimbali.

Ili mitaala hiyo ifanye kazi iliyokusudiwa, wameshauri serikali ijipange kikamilifu kwa kuhakikisha shule zinakuwa na vitendea kazi vya kutosha kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia. Mwishoni mwa wiki Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda aliwaeleza waandishi wa habari jijini Dodoma kuwa pamoja na mambo mengine rasimu ya mitaala mipya inapendekeza watoto wasome mpaka darasa la sita, kuweka mkazo wa ufundishaji katika kuandaa wanafunzi kujiajiri.

Mwenyekiti wa Taifa wa Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi Tanzania (TAMONGSCO), Leonard Mao, alisema mitaala hiyo ina nia njema ya kuandaa vijana wenye ujuzi na kwamba utawawezesha kujiajiri na kupunguza utegemezi katika jamii.

Vilevile, alisema vijana hao kupitia taaluma zao watasaidia serikali kufikia malengo ya kuwa na Tanzania yenye maendeleo ya viwanda ambayo ndiyo uti wa mgongo wa ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ulimwenguni.

"Vijana hao watakuwa na uwezo wa kujitegemea katika umri mdogo kwa kuwa wakimaliza elimu ya sekondari ya chini watakuwa na taaluma ambayo hata wasipoendelea elimu ya juu ya sekondari watakuwa na ujuzi wa kuanzia maisha," alisema Leonard.

Aidha, aliishauri serikali kuhakikisha kuna miundombinu ya kutosha ya kufundishia masomo ya amali, inayokidhi mahitaji ya wanafunzi wote ili wasikute wanafundisha masomo hayo kwa nadharia badala ya vitendo.

"Kwa kuwa hakuna mitihani ya darasa la saba ya kuwachuja ina maana wote wataingia sekondari, maana yake wanafunzi watakuwa ni wengi, ushauri wangu serikali ijipange, maana somo kama la ushonaji au kilimo ukilifundisha kwa nadharia peke yake halitokuwa na manufaa kwa wanafunzi," alisema.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Sera TAMONGSCO, Benjamin Nkonya, alisema mtaala huo ukitekelezwa ipasavyo utapunguza muda wa wanafunzi kukaa shuleni kutoka miaka tisa hadi miaka sita, kuwaunganisha na soko la kujiajiri na kuondoa dhana ya kusubiri kuajiriwa.

Alisema pia itachochea ukuaji wa uchumi wa nchi na kuipunguzia serikali gharama ya kuleta wataalamu kutoka nje ya nchi kuja kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa barabara.

Aidha, aliishauri serikali kuweka usimamizi mzuri katika utekelezaji wa mtaala hiyo ili ifundishwe vizuri na ilete matokeo tarajiwa kwa jamii na maendeleo ya nchi.

Pia kuweka mfumo wa kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa mitaala hiyo kwa kuwa peke yake haitoweza kutekeleza ipasavyo.

"Waige mfano wa nchi ya Netherland, kule katika elimu serikali yenyewe ni mwezeshaji na sekta binafsi ni mtekelezaji hii ikiletwa hapa nchini naamini itafanikisha adhma iliyowekwa ya kuandaa vijana kujitegemea," alisema.

Mmoja wa wamiliki wa Shule ya Msingi ya Uhuru Peak iliyopo Arusha, Gilbert Sarungi, alisema mitaala hiyo itawapa wanafunzi uhuru wa kuchagua wajikite katika taaluma gani tangu wakiwa wadogo na kuwapunguzia mzigo wa kusoma masomo mengi ambayo hawatoyafanyia kazi na kwamba wamejiandaa vyema kwenye utekelezaji.

Akizungumza jijini Dodoma, Waziri Mkenda alisema utaratibu huo mpya utaanzia kwa wanafunzi waliopo darasa la tatu mwaka huu na wa madarasa ya juu wataendelea na utaratibu uliopo wa kusoma mpaka darasa la saba.

Kwa upande wa sekondari alisema mwanafunzi ataanza kuipata akiwa na miaka 12 na watasoma elimu ya kawaida na amali zenye michepuo 11 ikiwamo sayansi, kilimo, michezo, TEHAMA, biashara, muziki, sayansi ya jamii, sanaa, ushonaji, chakula, lishe na lugha.

Aidha, alisema rasimu hizo zimependekeza masomo ya lazima ambayo mwanafunzi atatakiwa kuyasoma kuwa ni mawasiliano ya kitaaluma, historia ya Tanzania, maadili na somo la 'Basic Applied Mathematics'.

Alisema mitaala hiyo itaanza kutumika baada ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 toleo la 2023 kupitishwa na ikifanikiwa kupitishwa utekelezaji wake utaanza mwakani kwa kiasi kidogo na kasi itaongezeka taratibu.



Mfanyakazi wa usafi akisafisha mtaro wa maji ya mvua kandokando ya barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge Dar es Salaam jana. Baadhi ya mamalishe wa eneo hilo wamekuwa wakimwaga majitaka wanayosafishia vyombo na mabaki ya chakula na kusababisha mitaro hiyo kuziba. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Biteko: Tanzania, India zina uhusiano kiuchumi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amesema Tanzania na India zina uhusiano wa kidiplomasia na kiuchumi wa muda mrefu na jamii ya watu wenye asili ya India wamefanya uwekezaji mkubwa nchini.

Alisema watu wenye asili ya India wamefanya uwezekezaji mkubwa katika biashara, viwanda na sekta ya madini na kufanya biashara ya kuuza rasilimali hiyo pamoja na kuyakata ili kuongeza mnyororo wa thamani.

Waziri Biteko alisema hayo katika sherehe za maadhimisho ya miaka 77 ya Uhuru wa India, zilizoandaliwa na Watanzania wenye asili ya India, wanaoishi jijini Arusha, juzi.

Alisema Tanzania ina idadi ya watu wenye asili ya India zaidi ya 40,000 na kati ya hao kuna wageni ambao pasipoti za India ni kati ya 15,000 mpaka 20,000.

Pia alisema kwa mji wa Arusha pekee una jamii ya watu wa India 2,000 waliowekeza kwenye sekta mbalimbali ikiwamo za viwanda, madini na elimu.

"Tunawapongeza kwa kuwa kwa kuishi kwao hapa nchini kama Watanzania wenye asili ya India au kama wageni wanaokuja Tanzania kwa pasipoti za India wamekuwa mstari wa mbele kuwekeza na kuchangamkia fursa mbalimbali kwenye biashara.

"Tumeungana nao kusherehekea uhuru wao, kuwatia moyo na kuwatakia heri na sisi kama serikali tutawaunga mkono kwenye kila juhudi wanazozifanya na tunaliombea mema Taifa la India liendelee kuimarika na kuwa wamoja siku zote," alisema Biteko.

Naye Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Srikanta Pradhan, alisema Tanzania imekuwa sehemu salama pa kuishi na kufanya biashara na kuendeleza shughuli za utamaduni za nchi yao.

Vilevile, kutokana na uhusiano wa kidiplomasia, serikali ya nchi hiyo, imechangia zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni moja sawa na Shilingi trilioni 2.2 kwa ajili ya kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, aliwapongeza wananchi wa India na kuahidi kwamba akiwa kama mwakilishi wa wananchi katika Jimbo la Arusha, ataendelea kushirikiana nao.

"Nikiwa kama mbunge wa jimbo hilo, ninajivunia upendo na ushirikiano tuliokuwa nao kati yetu na watu wenye asili ya India," alisema.

Alisema watu hao wamekuwa mstari wa mbele kuchangia kwenye masuala ya maendeleo ikiwamo kutoa ajira nyingi hasa kwenye viwanda wanavyomiliki na kulipa kodi tena kwa uaminifu na uwapo wao unaleta matokeo chanya kwenye uwekezaji.



Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan.

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI

Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA

Usimamizi wa mirathi Na. 30/2021

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MUSSA JUMA GWANDI wa NKUHUNGU – MAILI MBILI

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA DANIEL PASCHAL LUZWILO NA SAIDI SOLOKA HOTTI

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **29 Mwezi 08 Mwaka 2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe **18** Mwezi **08 Mwaka 2023.**

---

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA LILILOKO DODOMA

MAOMBI MADOGO NA. 241 YA 2023

JOSEPH DICKSON ........................................MDAI

VERSUS

HAMIDU MALOWA ........................................MDAIWA 1
DEVIS DENIS MBOJE ........................................MDAIWA 2
CECILIA MGONJA........................................MDAIWA 3
ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPLIES(T) LTD..........MDAIWA 4

KWA:
HAMIDU MALOWA
DEVIS DENIS MBOJE
CECILIA MGONJA
ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPLIES(T) LTD

**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**Kwa kuwa** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili. **Kwa hiyo** unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba wilaya ya Dodoma wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe **08.09. 2023 saa 3:00 asubuhi.** Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe **18** ya mwezi wa **AGOSTI, 2023.**

# Waziri aelekeza kurekebishwa madirisha ya shule

**Na James Mwanamyoto**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, amemtaka fundi aliyepewa kandarasi ya kujenga Shule mpya ya Msingi ya Kona Nne, Halmashauri ya Wilaya Ushetu, mkoani Shinyanga, kurekebisha kwa gharama zake madirisha yote aliyoweka bila kuzingatia maelekezo ya serikali.

Ndejembi alimtaka fundi huyo kufanya marekebisho hayo haraka alipokagua ujenzi wa miundombinu ya elimu katika shule hiyo jana. Mradi umetekelezwa kupitia mradi wa BOOST katika Kijiji cha Bugomba 'A', Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, waziri akibaini dosari katika madirisha ya vioo yaliyowekwa shuleni.

"Ninaelekeza ndani ya siku 14 madirisha yote yaondolewe ili marekebisho yafanyike kwa ufanisi, tena kwa gharama za fundi na wasimamizi na si za Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu," Ndejembi aliagiza.

Naibu Waziri alisema amebaini madirisha hayo hayana wavu na hayajawekwa kwa viwango stahiki, hivyo marekebisho yafanyike na taarifa ya kukamilika kwa marekebisho hayo iwasilishwe kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Mkuu wa Wilaya ya Kahama na kwake ili kujiridhisha na utekelezaji wa maelekezo yake.

Pia alimtaka Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Kahama kufanya uchunguzi wa matumizi ya fedha katika ujenzi wa shule hiyo ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya watakaobanika kukwamisha jitihada za serikali za kuboresha miundombinu ya elimu nchini.

Pamoja na hilo, naibu waziri pia alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Hadija Kabojela, kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Mwalimu Jonas Mabusi ambaye ni msimamizi wa ujenzi na aliyekuwa Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Stella Solezi kwa kushindwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo.




Naibu Spika wa Bunge ambaye ni Mbunge wa Ilala, Mussa Azzan 'Zungu' (wa pili kulia), akikabidhi jiko la gesi kwa mmoja wa mamalishe, Editha Mahona, jijini Dar es Salaam jana, yaliyotolewa kwa ajili ya kutunza mazingira. Kushoto ni Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yazindua mashindano kuimarisha afya

**Na Maria Seme**

KATIKA kuhamasisha mazoezi ya kujenga mwili na kuimarisha afya, Benki ya CRDB imezindua mashidano ya Super League kwa timu zinazoundwa na wafanyakazi wake.

Michuano hiyo inayofanyika kwa mwaka wa tatu sasa, itashirikisha timu za mpira wa miguu na mpira wa pete, ikifanyika katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Inazishirikisha timu zinazoundwa na wafanyakazi kutoka idara, kanda na matawi ya benki hiyo nchi nzima.

Akifungua michuano hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba, alisema jana kuwa ni jambo jema kuona menejimenti inatoa fursa kwa wafanyakazi wake kufanya mazoezi ya mwili.

"Mnachokifanya Benki ya CRDB ni kitu kikubwa sana. Mnatoa mfano wa kuigwa na taasisi nyingine. Afya ndio mtaji muhimu kwa kila mfanyakazi, hivyo ni vyema kuilinda na mazoezi ndio namna ya uhakika wa kufanya hivyo. Hongereni sana Benki ya CRDB kwa kuwa na programu hii," alisema Komba.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo, alisema mafanikio endelevu si ya kifedha pekee, bali pia yanahusisha ustawi wa kila mmoja katika familia ya Benki ya CRDB.

"Kwa kukuza mazingira ambayo wafanyakazi wanaweka kipaumbele katika afya na furaha yao, tunaongeza ari ya uvumbuzi na ushirikiano hivyo kuimarisha utendaji wa benki kwa ujumla.

"Katika ulimwengu wetu wa leo, ni rahisi kusahau umuhimu wa kujijali na kudumisha usawa kati ya maisha ya kazi na maisha ya binafsi, hivyo tunapata fursa kama hii tuitumie vyema," alisema Nshekanabo.

Ligi hiyo, Nshekanabo alisema ni mwendelezo wa mpango wa Benki ya CRDB kuimarisha afya za wafanyakazi wake na anaamini kila mfanyakazi atashiriki michuano hiyo kwa namna moja au nyingine.

Sambamba na uzinduzi wa ligi hiyo, benki hiyo imefunga programu yake ya 'Ustawi, Afya na Furaha' (Wellness, Health and Fun) ambayo imefanyika katika kanda zake zote saba nchini kwa wafanyakazi kufanya mazoezi pamoja na kupima afya zao hasa magonjwa yasiyoambukiza.

Programu hiyo iliyoenda na kaulimbiu ya kuishi vyema, kufanya kazi vizuri, inalenga kuhamasisha ustawi wa mwili, akili na hisia za wafanyakazi wote wa Benki ya CRDB.

Katika viwanja hivyo, kulikuwa na wataalamu waliofanya vipimo tofauti vya afya kikiwamo cha tezi dume, BMI na shinikizo la damu, huku wakifundisha namna ya kukabiliana na msongo wa mawazo, ufanyaji wa mazoezi na ulaji salama.

"Msisitizo mkubwa tumeuweka katika afya ya akili, lengo kuu ni kuongeza uelewa wa kila mfanyakazi. Tungependa kuona kila mfanyakazi wa Benki ya CRDB anao ujuzi wa kuzitambua dalili za awali za msongo wa mawazo na hatua za kuchukua ili kuokoa jahazi lisizame iwe ni kwake mwenyewe, mwanafamilia yake hata jamii nzima," alisisitiza Nshekanabo.

Mbali na vipimo na ushauri wa kitaalamu uliotolewa, wafanyakazi walishiriki mazoezi tofauti kwa lengo la kuimarisha afya huku wakiendelea kufahamiana na kukuza uhusiano baina yao.

Nshekanabo alisema kwa kuwekeza katika ustawi na afya binafsi sio tu mtu anakuwa anaboresha maisha yake, bali pia anawahamasisha wanaomzunguka kufanya vivyo hivyo, jambo linalotoa chachu ya mafanikio kwa benki.

Mbali na kutenga siku ya mazoezi na vipimo vya afya kwa wafanyakazi wake na kuwahamasisha kushiriki michezo, Benki ya CRDB inayo miundombinu ya kisasa ya kufanyia mazoezi (gym) kwenye ofisi zake za makao makuu ambayo mkurugenzi huyo aliwataka wafanyakazi wote kuitumia kwa kuwa kila mmoja anayo rukhsa ya kuingia kufanya mazoezi ili kujenga na kuimarisha afya yake.

# Raia wa Burundi jela kwa kuingia nchini bila kibali

**Neema Msalaba na Queen Urio**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imewahukumu raia 59 wa Burundi kulipa faini ya Sh. 500,000 kila mmoja au kwenda jela kutumia kifungo cha mwaka mmoja, baada ya kukutwa na hatia ya kuingia nchini kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Ushindi Swalo baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote.

"Kwa kuwa mmekiri makosa yenu, mahakama inawahukumu kulipa faini ya Sh. 500,000 kila mmoja au kwenda jela mwaka mmoja ili iwe fundisho kwa wengine," alisema na kuamuru kuwa baada ya kumaliza kifungo chao, warudishwe nchini mwao.

Ilidaiwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali kutoka Idara ya Uhamiaji, Godfrey Ngwijo, kuwa raia hao wa Burundi walikamatwa Juni 13 mwaka huu, huko Jangwani, Dar es Salaam kwa kosa la kuingia na kuishi nchini kinyume cha sheria.

Aliomba mahakama kutoa adhabu kali kwa washtakiwa hao ili iwe fundisho na kukomesha matukio ya raia wa kigeni kuingia na kuishi nchini bila vibali.

Washtakiwa hao waliomba mahakama kuwaonea huruma na kusamehewa huku wakiomba warudishwe nyumbani kuliko kupewa adhabu.

HABARI KITAIFA

# Pandeni miti maeneo yenye miradi – Mkama

**Na Robert Hokororo,** UNGUJA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Dk. Switbert Mkama, ameitaka jamii kupanda miti kuzunguka maeneo yenye miradi ili kuhifadhi mazingira na kuifanya kuwa endelevu.

Aliagiza hayo mwishoni mwa wiki alipozuru na kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mfumo Mfumo Ikolojia Vijijini (EBARR) katika Wilaya ya Kaskazini 'A' Mkoa wa Kaskazini, Unguja, Zanzibar.

Akikagua visima, ujenzi wa majengo ya vituo vya wajasiriamali wa ufugaji, ushonaji, utengenezaji wa sabuni na vitalu nyumba katika Shehia za Jugakuu, Mbuyutende na Kijini, Dk. Mkama alisema ameridhishwa hatua iliyofikiwa.

Naibu Katibu Mkuu aliwahimiza viongozi wakiwamo masheha wa shehia hizo ambazo zimefaidika na miradi ya visima kuwasimamia wananchi kupanda miti na kuimwagilia.

"Binafsi nimeridhishwa na namna mnavyosimamia miradi hii na ninawapongeza masheha kwa kuisimamia na wananchi kwa kuipokea na kushiriki kikamilifu katika kuitekeleza, niwaombe mhakikishe inaendelea kuwa na ubora uleule," alisisitiza.

Kwa vile ujenzi wa majengo ya wajasiriamali wa ushonaji na uzalishaji wa sabuni utahusisha mashine na vifaa, Dk. Mkama alisema ni muhimu kuwapo mpango mkakati ili mradi uwe endelevu hata pale utakapokwisha muda wake.

Alisema vyerehani zitakazotolewa pamoja na vifaa vingine vikiwamo taa na mabomba ya maji vitahitaji matengenezo madogo na kulipiwa umeme, hivyo wanajamii waangalie namna ya kutoa huduma kwa mradi bila kusubiri serikali.

Naibu Katibu Mkuu pia alihimiza itolewe elimu ya ujasiriamali kwa watakaonufaika na mradi, pia kuna umuhimu wa kuwaelimisha kuhusu utunzaji wa miundombinu.

Mratibu wa EBARR Wilaya ya Kaskazini 'A', Alawi Haji Hija, alisema kupitia vitalu nyumba wananchi watafundishwa kilimo cha kustahimili ukame kwa kuwa watatumia maji ya visima kumwagilia mazao.

Pia alisema visima hivyo vitawasaidia katika upatikanaji wa huduma ya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ambayo walikuwa wanashindwa kuipata kutokana na changamoto ya ukame.

Pamoja na hayo, Hija pia aliongeza kuwa maeneo ambayo mradi unatekelezwa yamepimwa na tayari yamewekwa katika mpango wa matumizi bora ya ardhi ili yalindwe.

Hivyo, alisema kutajengwa uzio kuzunguka eneo la mradi ili kuweka ulinzi na kuutunza huku huduma ya maji ikiendelea kuwapo kwa wananchi wa maeneo hayo.

Sheha wa Shehia ya Jugakuu, Ali Abdallah Pili, alishukuru na kuipongeza serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuwapelekea wananchi hao Mradi wa EBARR.

Alisema wananchi wa shehia hiyo wanafarijika kujengewa visima na hivyo ambavyo vinatumia umeme wa jua, nishati ambayo ni ya gharama nafuu na wanayoweza kuimudu.

"Tunashukuru sana serikali kwa mradi huu na tumepata kikundi cha kutengeneza sabuni nzuri na umetupatia boti za kisasa za uvuvi ambazo wananchi wetu wanazitumia katika shughuli za kuvua samaki na hivyo kujipatia kipato," alisema.

Sheha huyo aliwashauri wanakikundi kuienzi na kuitunza miradi hiyo na kushirikiana kikamilifu katika shughuli mbalimbali zinazohusu miradi hiyo.

Miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Naibu Katibu Mkuu Dk. Mkama katika eneo la Matemwe, Wilaya ya Kaskazini 'A', imegharimu Sh. milioni 760.

Mradi wa EBARR unaofadhiliwa na Mfuko wa Nchi Zinazoendelea kupitia Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF), unatekeleza pia katika Wilaya za Mpwapwa (Dodoma), Simanjiro (Manyara), Mvomero (Morogoro) na Kishapu (Shinyanga).

Kupitia mradi huo, wananchi wa maeneo yenye ukame, wanawezeshwa kujipatia kipato kwa njia mbadala bila kujihusisha na vitendo vya uharibifu wa mazingira vikiwamo ukataji miti kwa ajili ya nishati na unyweshaji wa mifugo kwenye vyanzo vya kwa kuwa wanajengewa miundombinu kwa ajili hiyo.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Miradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Mhandisi Ramadhani Mtindasi, kuhusu mradi wa usambazaji wa majisafi katika maeneo ya Wazo Hill, Tegeta A na Goba alipotembelea mradi huo mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Vifaa kukabili tembo vyapelekwa Nachingwea

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI imepeleka vitendea kazi kwa ajili ya kufukuza tembo wanaovamia makazi ya watu ikiwa ni kujibu kero ya muda mrefu ya wakazi wa kata za wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, wanaosumbuliwa na wanyama hao.

Vitendea kazi hivyo ni ndege aina ya helikopta, gari na watumishi watakaohusika kuwaondoa wanyama hao na kuwarejesha msituni.

Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamedi Moyo, alisema ameyaeleza hayo wakati akizungumza kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani.

Alisema serikali imeshapeleka helikopta inafanya kazi ya kuwaondoa tembo kutoka maeneo wanayoishi wananchi na mazao yao yanayotokana na kilimo kwa kata tatu za Nditi, Kiparamnero na Mkoka wilayani humo.

Moyo alisema kwa kutambua uwepo wa changamoto zinazotokana na wanyama hao, serikali imeamua kuipeleka wilaya hiyo vitendea kazi ikiwamo helikopta, gari na watumishi watakaohusika na kazi ya kuwaondoa tembo hao na kuwarejesha maeneo wanayoishi ya msituni.

Aidha, alikieleza kikao hicho kuwa gari na watumishi hao inatarajia kuwasili wilayani humo leo.

Kwa mujibu wa mkuu wa wilaya, licha ya uwepo wa vitendea kazi na mradi wa kudhibiti wanyama hao uliozinduliwa wiki iliyopita mkoani Ruvuma, utahusisha mbinu za kuwadhibiti wanyama hao hatari na waharibifu mazao ya wakulima hususani tembo.

Alisema mradi huo utashirikisha vijana kutokea maeneo ya vijijini ni vizuri wakatafutwa vijana waadilifu watakaoleta ufanisi ulio mzuri na bora katika mradi huo ndani ya Wilaya ya Nachingwea na maeneo mengine.

"Kuzinduliwa kwa mradi huu tutapita katika maeneo yenu kutafuta vijana angalau kumi, watapewa mafunzo ya mbinu za kuwazuia tembo ndani ya wilaya yetu," alisema Moyo.

Aidha, Moyo waliwaomba madiwani kusaidia kuwapata vijana wenye nidhamu na waadilifu kwa ajili ya kupata ajira itakayowasaidia kujipatia kimapato na kulinda rasilimali za wakulima kwenye mazao yao.

Awali wakiwasilisha kilio cha wanyama hao, madiwani na kata wanazotoka kwenye mabano, Ally Ahamadi Mtile (kata ya Kiparamnero), Saidi Mohamedi Kuleni (Kata Mkoka) na Kaisi Juma Lukanga (Kata ya Nditi) walitaka kufahamu jitihada zinazochukuliwa na serikali katika kuwaondoa tembo wanaohatarisha usalama wa maisha na mazao katika maeneo yao.

Walisema hivi sasa wanyama hao wamekuwa tishio kwa usalama wa wananchi na mazao yao na mwezi huu wananchi wawili wamepoteza maisha kwa kukanyagwa na wanyama hao, mmoja akiwa shambani na mwingine akiwa anarejea nyumbani akitokea mazikoni kijiji jirani.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
18.08.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **21.08.2023 hadi 28.08.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Bandari ya Dar Es Salaam** kuelekea **Mzenga**, gari hilo lenye namba za usajili

**NRB97300 / NRB54202**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | Mita | **22.5** |
| Upana | - | Mita | **5.30** |
| Kimo | - | Mita | **4.80** |

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam** hadi **Mzenga** kupitia **Barabara ya Mandela, Barabara ya Morogoro** gari litasafiri muda wa mchana **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**.

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi Ligi Kuu Bara bado wanachechemea

**LIGI** Kuu Bara msimu wa 2023, mwishoni mwa wiki iliingia mzunguko wa pili kwa baadhi ya timu huku Yanga ikiwa ni klabu pekee ambayo haijacheza mechi hata moja tangu kuanza kwa ligi hiyo Agosti 15, mwaka huu.

Hata hivyo, kuna sintofahamu kwa nini Yanga haijacheza mechi hata moja, ingawa sababu tajwa ni kupewa muda wa kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, dhidi ya ASAS ya Djibouti iliyochezwa jana.

Katika hilo kumezuka maswali mengi, iweje Yanga yenyewe isicheze mechi angalau moja kama ilivyo kwa Azam FC na Singida Fountain Gate ambazo nazo zilikuwa na kibarua kama hicho kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Tena kwa Azam FC ndiyo timu iliyostahili kupewa mapumziko zaidi kwani, mchezo wake wa raundi ya awali imesafiri kwenda kucheza nchini Ethiopia dhidi ya Bahir Dar Kenema FC, kungali Yanga na Singida Fountain Gate, zenyewe zimecheza hapa hapa nchini.

Hivyo, kuna haja Bodi ya Ligi nchini (TPLB), kuandaa ratiba rafiki kwa kila klabu bila kuangalia ukubwa wa timu ama ukongwe wake ili mwisho msimu kupata bingwa aliyestahili na si wakubebwa.

Hata hivyo, pamoja na changamoto hiyo ya ratiba bado kuna tatizo kubwa la waamuzi kushindwa kufanya maamuzi sahihi katika baadhi ya mechi ikiwa ndiyo kwanza mechi za mzunguko wa pili.

Kama ilivyokuwa katika mchezo wa fainali wa Ngao ya Jamii uliopigwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga na mwamuzi Jonisia Rukyaa kushindwa kutoa penalti baada ya mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis kuchezewa madhambi ndani ya 18 na kiungo wa Yanga, Khalifa Aucho, makosa kama hayo yameendea kujitokeza Ligi Kuu.

Katika mchezo wa Simba tena dhidi ya Mtibwa Sugar, mwamuzi mwamuzi Nassor Mwinchui, alishindwa kutoa adhabu ambayo dhahiri ilistahili kuwa penalti baada ya Kibu Denis tena kuchezewa madhambi ndani ya 18.


Hiyo ni baadhi ya michezo ambayo tumebaini bado kuna shida kubwa kwa waamuzi, hivyo kuna haja kwa TPLB kuigeukia Kamati ya Waamuzi ili kuliondoa tatizo hilo.

Lengo letu si kuwahukumu waamuzi hao, bali nikutaka kuikumbusha TPLB na kamati ya waamuzi kuwa makini na kuzidi kuwakumbusha kila wakati waamuzi kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwani ni wazi yapo makosa ambayo ni ya kibinadamu wanayofanya, lakini wapo pia baadhi ya waamuzi wanaofanya makosa hayo kwa dhamira yao ovu wenyewe.

Hivyo, kwa kuwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), wiki iliyopita waliendesha semina ya pamoja kujadili namna ya kuondosha vitendo kama hivyo michezoni, watapewa ushirikiano wa kutosha.

Lengo letu ni kuona tunakuwa na msimu bora zaidi kuwahi kutokea ili ligi yetu izidi kupanda viwango kutoka nafasi ya tano bora Afrika na kuingia tatu bora, hivyo hatuwezi kufika huko kama waamuzi wakiendelea kuamua matokeo yao badala ya timu iliyoonyesha ubora.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wachezaji wanaowatishia waamuzi wa kike wachukuliwe hatua kali

Na Adam Fungamwango

**KUMEKUWA** na baadhi ya wachezaji kuwatowaheshimu waamuzi wa kike kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na hata Ligi ya Championship.

Wakati dunia sasa inaondokana na mfumo dume, bado kuna baadhi ya wachezaji wameonekana kuwa na tabia ya kuwazingira, kuwakemea, kuwadhihaki na kuwatisha waamuzi wa kike.

Utaona kabisa kuwa hata kama ni kweli kuna kosa la dhahiri, lakini mchezaji anakasirika na kumfuta mwamuzi kwa nia ya kumtisha na kumfanya aonekana amekosea, kitu ambacho si sahihi.

Hata Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi, Nassor Hamduni, amelizungumza hili katika mahojiano maalum na Nipashe hivi majuzi.

Hamduni, pamoja na kwamba alilielezea suala hili kwa ujumla, lakini alisema hasa waamuzi wa kike wamekuwa wakikumbwa na changamoto hii na lengo ni kuwaondoa mchezoni, kuwafanya waonekane hawafai.

"Hii si vizuri hata kidogo, na kwa sababu inaonekana kwenye televisheni, wengine wakiona wanaendelea na tabia hii, nawapongeza sana waamuzi wetu kwa sababu nao hawaingii kwenye jazba ya wachezaji badala yake wanafuata sheria na kanuni inavyomwelekeza, vinginevyo kama na wao wangekuwa wanajibu mapigo na wao ndiyo wanaoamua kila kitu uwanjani, sidhani kama hali ingekuwa nzuri," anasema. Ana maana kuwa yale maneno makali ambayo wachezaji wamekuwa wakiwatolea waamuzi wa kike, kama na wao wangekuwa wanajibu kwa kutumia tu kadi zao mkononi, kungekuwa na idadi kubwa ya wachezaji ambao wangekuwa wanaadhibiwa.

Nadhani waamuzi hao nao kwa sababu wameshachezesha mechi nyingi tena tangu huko madaraja ya chini ambako ndiyo kuna vimbwanga na tabia za kila aina za wachezaji, wameshakomaa na kujionea kawaida tu.

"Waamuzi wetu wanatumia busara sana kwa sababu nchi zingine huwezi kumzonga, kumshika, wala kumzunguka mwamuzi ukimfokea, hili jambo mimi naomba wale wachezaji wenye tabia hiyo waiache kwa sababu yeye akishatoa maamuzi hata ufanye nini hawezi kubadilisha," anasema bosi huyo wa waamuzi.

Ni kweli mwamuzi akishatoa maamuzi yake, yawe wamenufaisha upande mmoja na kuumiza mwingine, yako sahihi au si sahihi, lakini hawezi kubadilisha.

Waamuzi wa Tanzania watakuja kubadilisha maamuzi yao pale tu zitakapoanza kutumia VAR, lakini kwa sasa ambapo wanatumia kuona matukio na wakati mwingine kuhisi tu, hawawezi kubadilisha hata kama wachezaji watamfokea, kumtisha au kugomea na kutoka uwanjani.

Binafsi, nawapongeza sana waamuzi wa kike kwani ukiangalia mechi mbalimbali wanachezesha kwenye mazingira magumu kuliko wa kiume.

Baadhi ya wachezaji wanataka kuwafanya wasijiamini, waonekane hawajui kuchezesha au wanavurunda kwa kutaka kulalamika kwenye kila tukio.

Hii ni mbinu ya kutaka kuwafanya baadhi ya mashabiki wanaoangalia kwenye televisheni kuanza kumjadili.

Katika uzoefu wangu wa kuangalia soka nimegundua kuwa mwamuzi pekee wa kike ambaye hachezewi sana na anaogopwa na wachezaji ni Jonisia Rukyaa, labda kutokana na kwamba wengi wameshamfahamu kuwa hayumbi wala hayumbishwi kwenye misimamo wake na huwa mkali pale mchezaji anapoonekana kujaribu kumfanya asiitende kazi yake vizuri.

Wengine wamekuwa na changamoto kiasi cha kuonekana kama kutikiswa hivi na wachezaji. Rai yangu kwa wachezaji ni kwamba wafuate kile kilichowapeleka uwanjani na kama malalamiko kuna nahodha ambaye anaweza kwenda kuongea naye.

Pia TFF kupitia kamati zake kuanza kutoa adhabu kwa wachezaji wanaoonekana kuwazonga mara kwa mara waamuzi, hasa wa kike ili waendelee kuchezesha vizuri na kuwavutia wengine wanaoingia kwenye tasnia hiyo.

HABARI KITAIFA

# Bodi Parole yakataa pendekezo la kuwaachia huru wafungwa 16

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

BODI ya Taifa ya Parole imesema haijaridhidhwa na mapendekezo ya kuwaachia huru wafungwa 16 walioomba kuachiwa huru kupitia Sheria ya Parole.

Wafungwa hao ni waliokutwa na makosa ya ujangili na mauaji.

Katika kikao cha 48 cha bodi hiyo, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Balozi Khamis Kagasheki, aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa wafungwa hao wameshindwa kukidhi vigezo kutokana na kukutwa na makosa hayo na kuharibu rasilimali za utalii wa nchi.

"Bodi haijaridhia maombi ya wafungwa 16 kuachiwa huru, na hii imetokana na kukutwa na makosa ambayo hawapaswi kuachiwa huru,"alisema Balozi Kagasheki.

Alifafanua kuwa bodi hiyo inawasilisha majina 12 ya wafungwa waliokidhi vigezo vya kuachiwa huru kupitia sheria hiyo kwa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili kuridhia uamuzi hayo.

Aliwataka wafungwa hao watakaoachiwa huru kubadilika kitabia na kuwa raia wema.

"Jeshi la Magereza linaendelea kuweka utaratibu wa kutoa elimu kuhusiana na Sheria ya Parole kwa jamii ili kuitofautisha na ile ya msamaha wa Rais ambao nao kuna baadhi ya wafungwa huwa wanaachiwa huru.

"Jamii iwapokee watu hawa ambao wataachiwa huru kwa sababu mpaka kupitishwa na bodi hiyo, maombi yamepita sehemu mbalimbali, ikiwamo kuuliza ndugu, waathirika wa makosa waliotendwa na watu hao kama wapo hai pamoja na kamati za wilaya, mkoa hadi taifa," alisema.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza na Kaimu Kamishna wa Sheria na Uendeshaji wa Magereza, Boyd Mwambingu, alisema kuna mambo ambayo wameangalia kwa wafungwa hao walioomba.

Aliishukuru Bodi ya Parole kwa kutoa uamuzi kwa kuangalia maslahi mapana ya nchi.

Awali, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Ramadhan Nyamka, alisema bodi hiyo itaendesha kikao hicho kwa kuzingatia sheria hiyo na kusisitiza haki itatendeka katika utoaji uamuzi.



Mwendesha guta akiwa amelisheheni mzigo wa vipande vya magodoro katika eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana na kumfanya ashindwe kuona nyuma kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uuzaji Tanga Cement wagonga mwamba tena

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Ushindani wa Biashara (FCT) limezuia kwa mara nyingine uamuzi wa Tume ya Ushindani (FCC) wa kuruhusu kampuni ya Scancem International DA inayomiliki kampuni ya Saruji ya Twiga kununua hisa za Kampuni ya Saruji ya Tanga kamka uliofanyika Februari 28, mwaka huu.

Uamuzi huo ulifanyika baada ya ule wa awali kukatazwa na FCT Septemba, 2022 baada ya kufunguliwa kwa shauri na baadhi ya wadau kuwa uuzaji wa hisa hizo ambao ungesababisha muunganiko kati ya Twiga Cement na Tanga Cement ungesababisha athari za kibiashara.

Miongoni mwa athari zilizowasilishwa mbele ya baraza hilo na wadau hao ni kuwapo kwa ukiritimba katika soko kutokana na mzalishaji mmoja kuwa na asilimia nyingi na kuwapo kwa uwezekano wa kupanga bei ya bidhaa na kusababisha kuathiri watumiaji.

Pamoja na kuwapo kwa katazo hilo, FCC ilitangaza tena kuwa muunganiko huo baina ya kampuni hizo mbili unarejewa na kukaribisha wadau kutoa maoni, jambo ambalo lilisababisha baadhi ya wadau kutaka jambo hilo lizuiwe kisheria na kwamba linakiuka sheria na uamuzi uliotolewa na FCT ambacho ni chombo cha juu katika utatuzi wa migogoro ya kibiashara.

Kutokana na hali hiyo, kampuni ya Saruji ya Chalinze ilikata rufani FCT kupinga uamuzi wa FCC kuruhusu muunganiko huo na baraza hilo limetoa uamuzi unaozuia kuendelea kwa muunganiko huo huku likisisitiza kwamba umezuiwa kisheria.

Katika hoja zake za rufani, mrufani alidai kuwa FCC ilikosea kisheria kwa kuruhusu muunganiko ambao ulikatazwa na FCT katika uamuzi wake uliotolewa Septemba 23, 2022. Pia FCC ilidaiwa ilikosea kisheria kwa kuitisha upya mchakato wa muunganiko wakati shauri hilo lilishatolewa uamuzi.

Hoja nyingine katika rufani hiyo ni kwamba FCC ilikiuka sheria kwa kudai kuwa katazo la FCT halizuii moja kwa moja, hivyo si la kudumu kwa kuzuia muungano wa kampuni hizo.

Hata hivyo, mjibu rufani namba moja, FCC na Wakili Mkuu wa Serikali ambaye ni mjibu rufani namba mbili, waliibua hoja kwamba mchakato wa Februari, 2023 ulifanyika baada ya kufanya upembuzi yakinifu wa kisoko kuwa hakuna madhara yanayoweza kujitokeza.

Pamoja na hoja hiyo, FCT katika uamuzi wake imesema FCC ilifanya uchunguzi na kutoa ripoti ambayo inaonyesha dhahiri kwamba muunganiko unaokusudiwa unaweza kuwa na athari katika ushindani. "Baada ya kujiridhisha kuwapo kwa athari za kiushindani na uchumi kama muunganiko huu utapata kibali, mjibu rufani namba moja aliendelea na mchakato... Baada ya kufanya tathmini na kuangalia uzito wa hoja, Baraza (FCT) limeridhika kwamba kama muunganiko huu utapitishwa bila masharti yoyote, kuna uwezekano wa kuathiri watumiaji wa bidhaa, hivyo muunganiko huo umezuiwa," ilieleza sehemu ya hukumu hiyo.

Jaji Maghimbi pia alisema pamoja na kukubaliana na hilo kwamba kuna uwezekano wa kubadilika kwa nguvu za soko, haridhiki na muda mfupi uliotolewa katika mchakato. Kwa mantiki hiyo, alisema haridhiki na mabadiliko hayo ambayo yangelifanya Baraza kurejea uamuzi wake wa awali kuhusu muunganiko huo.

Aidha, Jaji Maghimbi katika uamuzi huo, alieleza kushangazwa na FCC ambayo imepewa jukumu la kusimamia ushindani kwenye masuala ya kiuchumi kwa maslahi ya watumiaji wa bidhaa, kudharau nguvu za kisheria za Baraza kwa kuendelea na mchakato ambao ulizuiwa kisheria.

"Lazima nisisitize kwamba kitendo kilichofanywa na wajibu rufani hakikuakisi ujumbe chanya kwa umma na kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika nchi yetu kwa kuitisha upya mchakato katika jambo lililokuwa limezuiwa. Jambo hilo limefanywa kinyume dhidi ya uwapo wa utawala wa sheria," alisema Jaji Maghimbi.

"Sababu kubwa inayowafanya wawekezaji kuona nchi yetu ni 'paradiso' katika uwekezaji ni uwapo wa utawala wa sheria, kuheshimu sheria, kutokuwapo upendeleo na na usawa mbele ya sheria.

Hili halina budi kuheshimiwa kwa namna yoyote pasipo kumpendelea mwekezaji mmoja kwa sababu inaweza kusababisha madhara hasi.

Jaji Maghimbi aliionya FCC kwamba FCT ni chombo cha juu katika kusimamisha sheria na kutatua migogoro inayojitokeza kibiashara, hivyo inapaswa kuheshimu uamuzi wa awali wa Septemba 2022 ambao ulikataza muunganiko huo.

Pia Jaji Maghimbi katika hukumu hiyo alimuuliza Wakili Mkuu wa Serikali kama kuanzisha mchakato mpya wa Februari 2023 wakati kuna hukumu ya Septemba 2022 kama ilikuwa njia sahihi na alikiri kuwa haikuwa sahihi kufanya hivyo.

Aidha, katika uamuzi huo, Jaji alitoa amri kwamba FCC iombe marejeo ndani ya siku 30 tangu Julai 6, mwaka huu, kama inataka kuanzisha mchakato mpya kitu ambacho mpaka sasa hakijafanyika na muda umemalizika.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed






Mkazi wa Mbezi, Joyce Massaba, akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni moja kutoka kwa Meneja wa Wateja Maalum Tigo Pesa, Mary Rutta, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuibuka mmoja wa washindi wa promosheni ya Cha Wote. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia atoa tuzo maalum kwa benki

**Na Maria Seme**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa tuzo maalum kwa Benki ya NMB katika kutambua mchango na utendaji mkubwa wa taasisi hiyo ya fedha nchini.

Katika kikao kazi cha wenyekiti wa bodi na watendaji wakuu wa taasisi za umma kinachofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Arusha (AICC) juzi, Rais Samia alisema kuwa mbali na kuwapongeza waliofanya vizuri, serikali pia itafanya tathmini ya utendaji wa taasisi na mashirika mengine ya Tanzania.

"Kupitia mashirika, serikali inaweza kukusanya fedha nyingi za kutosha kujazia upungufu wa bajeti ya nchi na hivyo kuipunguzia serikali mzigo wa kwenda kukopa nje," alisema.

Rais Samia alisisitiza taasisi zingine ziige mfano wa zile zinazochangia kasma ya Taifa kupitia gawio serikalini.

"Ni muhimu sana Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe inasimamia ipasavyo sheria na kanuni zilizopo katika kuhakikisha taasisi za umma zinajiendesha kwa tija na kuipunguzia serikali mzigo wa gharama za kuziendesha," aliagiza Rais Samia.

Benki ya NMB ilitoa gawio la Sh. billioni 45.5 serikalini katika mwaka wa fedha uliopita.

Pamoja na kutoa pongezi kwa Benki ya NMB, Rais Samia pia alimkabidhi cheti cha mlipa gawio kubwa serikalini sekta ya kibenki Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo ya fedha, Ruth Zaipuna.

Kwa mujibu wa Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, serikali inamiliki asilimia 31.8 ya hisa katika Benki ya NMB.

"Tumetoa tuzo kwa taasisi zilizofanya vizuri ili kuleta changamoto katika kujifunza sisi sote na ili taasisi zingine ziwe na wivu wa kusonga mbele ndipo tuweze kuisaidia nchi yetu," alisema Mchechu.

Kwa mujibu wa Msajili wa Hazina, serikali imewekeza zaidi ya Sh. trilioni 73 katika taasisi za umma na ni jukumu lao kuhakikisha fedha hizo zinazaa matunda makubwa katika kukuza uchumi wa nchi.

"Tunatarajia kuwa siku za mbeleni pamoja na kuwa na orodha ya sifa ya taasisi zinazofanya vizuri, baadaye pia tungeweza kuwa na orodha ya aibu kwa taasisi zinazofanya vibaya lakini hatutarajii kufika huko, kutokana na maboresho makubwa tunayofanya kwa taasisi hizi kwa sasa," alisema Mchechu.

Jumla ya taasisi 248 zimeshiriki mkutano huo wa kwanza wa mwaka wa kikao kazi cha wenyekiti wa bodi na watendaji wakuu wa taasisi za umma ukiwa na washiriki zaidi ya 600.

# TAKUKURU yabaini shida utendaji wa AZAKI

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro imesema Asasi za Kiraia (AZAKI) zinazofanya shughuli zake mkoani hapa, hazikidhi matakwa ya serikali na miongozo ya uwasilishaji taarifa zao na kuzitaka kufanya hivyo kama utaratibu unavyoelekeza.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro, Manyama Tungaraza, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotoa taarifa yake kwa umma kuhusu utendaji kazi katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu.

Alisema TAKUKURU ilifanya uchambuzi wa mfumo wa mianya ya rushwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa kutumia mfumo wa 'Force Account' katika halmashauri za mkoa huo na kubaini kasoro mbalimbali na kutoa maelekezo kwa wahusika.

Alisema pia walifanya uchambuzi wa mfumo wa utekelezaji wa maazimio ya udhibiti wa mianya ya rushwa katika utendaji wa kazi za AZAKI na kubaini kuwa nyingi hazikidhi matakwa ya serikali na miongozi ya uwasilishaji wa taarifa.

Alizitaja asasi za Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero zilionesha kuwapo kasoro hizo na halmashauri hiyo imeshauriwa kuhakikisha asasi zinazoanzishwa zinakidhi matakwa ya serikali na miongozo ya uwasilishaji wa taarifa zao.

Kuhusu ushirikishaji wadau katika utatuzi wa kero kupitia Programu ya TAKUKURU Rafiki ambayo ilishazinduliwa na kuanza utekelezaji wake mwezi Februari mwaka huu, kiongozi huyo alisema imeweza kuwafikia wananchi wanaoishi katika kata 36 za Mkoa wa Morogoro.

Tungaraza alisema katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu, programu hiyo imeongeza uelewa kwa wananchi kwa kuwajengea ujasiri wa kuibua na kutoa kero mbalimbali ambazo kama zingeachwa zingeweza kusababaisha vitendo vya rushwa kushamiri.

Alitaja eneo lingine ni kujenga na kuimarisha uhusiano mazuri kati ya TAKUKURU na watoa huduma wa taasisi mbalimbali katika utatuzi wa kero zilizowasilishwa kwao na kuzifanyia kazi kwa wakati.

Tungaraza alitaja eneo lingine ni kuongeza dhana ya uwajibikaji katika utumishi wa umma hasa katika kuhakikisha huduma zinazotolewa na taasisi husika zinatekelezwa kwa ufanisi.

Tungaraza alisema taasisi hiyo itaendelea na utekelezaji wa programu hiyo kwa kufikia kata ambazo bado hazijafikiwa kwa ajili ya kubainisha kero mbalimbali zinazowakabili wananchi na kuzitafutia ufumbuzi kwa kuwekeana mikakati na wahusika.

"Matarajio ya programu hii ni kuibua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi katika maeneo yao ili zijadiliwe na kutatuliwa na wahusika kwa wakati," alisema.

Mjumbe wa Bodi wa Umoja wa Mashirika ya Yasiyo ya Kiserikali mkoani hapa, Divunyagale Juma, alisema ni muhimu asasi hizo kuanza kubadilika na kuwasilisha taarifa zao kama utaratibu unavyoelekeza.

"Huu ni utaratibu uliowekwa na serikali wa kuwasilisha taarifa za utendaji wa kazi, hivyo kila asasi ni muhimu kufuata ili shughuli zinazofanyika zifuatwe," alisema Divunyagale.

# Ubalozi China waombwa dirisha maalumu la Visa kwa wanafunzi

**Na Joseph Mwendapole**

MKURUGENZI wa Global Education Link, Abdulmalik Mollel, ameomba Ubalozi wa China nchini kufungua dirisha maalumu kwa wanafunzi Watanzania wanaoomba Visa kwenda kusoma nchini humo.

Mollel amesema kuna idadi kubwa ya wanafunzi wa Tanzania ambao wangependa kwenda kusoma China, hivyo dirisha hilo litawarahisishia wanaoomba Visa wapate kwa haraka.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya kuwaaga vijana 46 wa Tanzania wanaokwenda kusoma fani mbalimbali China kwa ufadhili wa serikali ya nchi hiyo, fursa ambayo hutolewa kila mwaka.

Mollel alisema China ina vyuo vingi bora ambavyo vinatoza gharama za kawaida kumwezesha kila Mtanzania anayetaka kwenda kusoma nchini humo kumudu gharama hizo za masomo.

"Kama mwanafunzi anataka kusoma vyuo vyenye mchanganyiko wa tamaduni, vyenye mahudhurio makubwa ya wahadhiri, vyenye usalama wa kutosha na gharama ndogo, basi China ni chaguo bora kwa sababu haya yote yapo.

"Kwahiyo, wakati wowote serikali inapofikiria kuwapeleka wanafunzi nje ya nchi, hata kupitia mpango wa ufadhili wa bodi ya mikopo, bajeti ileile mnayowapa wanafunzi kwa vyuo vya Tanzania inaweza kukidhi gharama za vyuo vya China," alisema.

Mollel alisema kwa miaka mitatu mfululizo, China ilikuwa imefunga mipaka yake, hivyo wanafunzi kushindwa kwenda nchini humo, lakini anashukuru kwamba hali imerejea kama kawaida na wanafunzi wa Tanzania wameanza kwenda nchini humo.

Alisema wanafunzi wanapaswa kuripoti vyuoni mwezi Septemba, hivyo aliomba ubalozi huo kuwapa upendeleo wa Visa za haraka wanafunzi wanaokwenda kusoma nchini humo. "Tuwape fursa wanafunzi kuomba visa mtandaoni mapema kwa sababu tarehe 15 Septemba wanatakiwa kuripoti vyuoni. Kwahiyo, wanatakiwa kupata kabla ya muda huo. Sasa tukiwacheleweshea wanaogopa kuomba vyuo vya China," alisema.

"Na hili linawezekana kwa sababu Idara ya Visa imekuwa ikitoa ushirikiano mkubwa sana tunapokwenda kuomba Visa na hata sasa wanafunzi wangu wanaopitia Global Education Link kwa sasa wanoomba Visa, hakuna anayekwama. Tunapata ushirikiano mkubwa sana na msaada mkubwa," alisema.

"Lakini kuomba Visa mtandaoni ndiyo inachukua muda mrefu. Ninawaomba mfungue dirisha maalum kwa wanafunzi wanapoomba Visa wawe wanapata kwa urahisi na kwa haraka. Tukiweza kufanya hili tutakuwa tumewamasisha wanafunzi wetu wengi kwenda kusoma China," alisema.

Mollel alisema kutokana na uhusiano mwema uliopo baina ya Serikali ya Tanzania na China, GEL itaendelea kushirikiana na serikali ya nchi hiyo kuhamasisha wanafunzi wengi wa Tanzania kwenda kusoma vyuo mbalimbali vya nchi hiyo.



HABARI KANDA KASKAZINI

# LATRA yazima mgomo bajaji, daladala, yatoa maagizo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Mkoa wa Arusha, umefanikiwa kumaliza mgomo wa daladala uliodumu kwa siku tatu katika jijini hapa na kusababisha adha kwa wananchi, wafanyabiashara na wanafunzi.

Pia imepiga marufuku chombo cha usafiri aina ya bajaji kufanya biashara ya kupakia abiria kama daladala badala yake, wametakiwa kukodishwa.

Agizo hilo lilitolewa jana na Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Arusha, Joseph Michael, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo akitolea ufafanuzi mgomo huo.

Hata hivyo, aliwahakikishia wananchi kuwa hakuna mgogoro wowote utakaotokea kwa sasa baina ya daladala na bajaji mkoani hapa.

Alisema kutokana na kukabiliana na mgomo huo, tayari mamlaka hiyo imeshatangaza vituo vipya 50 vya daladala ambavyo vitatumika kupakia na kushusha abiria.

Aidha, alisema hadi sasa ni bajaji 700 pekee zenye leseni ya mamlaka hiyo, ndiyo zitaruhusiwa kufanya biashara hiyo na bajaji zisizo na leseni hazitaruhusiwa.

Alisema zitakazobainika zitakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria iwapo kama zitaonekana zinafanya kazi kinyume cha sheria.

Pia alisema LATRA, imepiga marufuku magari yote madogo aina ya daladala kuingia mjini na abiria na gari zitakazoruhusiwa kubeba abiria mjini ni magari makubwa aina ya costa, kwamba kuanzia Agosti 21 mwaka huu hatua kali zitaanza kuchukuliwa kwa watakaokiuka.

Nao baadhi ya wakazi wa Jiji la Arusha walipongeza uamuzi wa mamlaka hiyo ya kupanga vituo vipya vya daladala, pia kupiga marufuku daladala kupakia abiria mjini kutokana na usumbufu unaosababisha msongamano mjini.

Hamidu Nasari, mkazi wa Mbauda, alisema uamuzi huo unalenga kuboresha usafiri ndani ya Jiji la Arusha na utasaidia kuondoa msongamano unaosababisha usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara.



Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatuma Mwasa (wa pili kulia), akikabidhi mtungi wa jiko la Oryx kwa mmoja wa wanufaika wa msaada, wakati wa ugawaji wa mitungi ya Oryx Gas na majiko yake bure kwa wananchi wa makundi mbalimbali iliyotolewa na kampuni hiyo, mkoani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaweka mikakati korosho itambe soko la dunia

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI kupitia Wizara ya Kilimo imeweka mpango mkakati wa kuhakikisha inafanya maboresho kwenye sekta ya kilimo kwa zao la korosho ili iendane na kasi ya soko la dunia kwa biashara ya zao hilo.

Mpango mkakati huo unelenga kufikisha Sh.trilioni 21.8 kutoka kiasi cha Sh.trilioni 17.8 kwenye uboreshaji wa zao hilo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alibainisha hayo jana kwenye mkutano mkuu wa wadau wa korosho kwa mwaka 2023 uliofanyika jijini Tanga na mkutano huo uliwashirikisha viongozi, wadau wa zao hilo, kampuni za ununuzi kutoka mikoa inayolima zao hilo.

Mavunde alisema takwimu za soko la dunia zinaonyesha kwamba biashara ya korosho kwa msimu uliopita biashara iliyofanyika ni Sh.trilioni 17.8 na inakadiriwa ifikapo mwaka 2018, biashara ya zao hilo itafikia zaidi ya Sh.trilioni 21.8 kwa dunia.

"Tukifanya maboresho na uwekezaji kuanzia kwenye utafiti na pamoja na kuwawezesha wakulima kulima kilimo chenye tija kuna fursa kubwa sana duniani kwa zao la korosho na sisi kama serikali tunaona hii ni fursa na tutaitumia vizuri ili wakulima wetu wanufaike kwa kilimo hiki," alisema Mavunde.

Alisema kutokana na mpango huo serikali bado inaendelea kufanya maboresho makubwa katika zao la korosho.

Alisema: "Bajeti ya sekta ya kilimo tumeweza kuwapa wakulima wa korosho pembejeo na tumewapatia miche bora ya korosho na kwa bajeti ya mwaka huu Sh.bilioni 50 zimetengwa." Kadhalika, alitoa agizo kwa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kusajili wakulima kwenye ngazi ya wilaya na kata ili zoezi la uboreshaji wa kilimo cha zao hilo lifanikiwe.

"Hakikisheni mnawasajili wakulima kuanzia ngazi la wilaya na kata ili tuweze kwenda kwa haraka kwa kuwa hili ni jukumu la bodi kuongeza wasimamizi," aliongeza.

Alisema wakulima watapata nafasi ya kujua aina ya ukulima wao, mashamba, pembejeo wanazopatiwa pamoja na miche ili iwasaidie.

Pia alitoa rai ya kuvutia na kuhamasisha uwekezaji wa ubanguaji na usindikaji wa korosho kwa kutenga eneo la kutosha kwa ajili ya shughuli hasa katika Kijiji cha Maranje, Kata ya Mtindiko kwenye Halmashauri ya Mji wa Nanyamba mkoani Mtwara.

Alisema katika eneo hilo kuwa kuna ekari 1,575 ambazo zimetengwa na zitatumika kujenga kongani la viwanda kwa mwaka huu wa fedha.

# Mradi wa kitita waokoa maisha ya watoto, wajawazito

**Na Allan Isack,** BABATI

WATAALAMU wa afya kutoka Mkoa wa Manyara, wamefanikiwa kuokoa maisha ya watoto wachanga zaidi ya 100 na wajawazito 25 waliokuwa wako hatarini kupoteza maisha kwa kukosa huduma bora za kitaalamu.

Wataalamu hao wamefanikiwa kuokoa maisha ya watu hao baada ya kuanza kwa utakelezaji wa mradi wa kitita cha uzazi salama ulianzishwa kwa lengo la kuboresha huduma za afya hasa kupunguza vifo kwa wajawazito na watoto.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kutembelea Hospitali ya Wilaya ya Babati, kukagua jengo la mama na mtoto, Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk.Ntuli Kapologwe, alisema mradi huo umekuwa msaada kwa wanawake na watoto na umeleta matokeo chanya.

"Tulichofurahishwa tangu mradi huu, umeanza kutekelezwa katika mkoa wetu wa Manyara, umesaidia kuokoa maisha ya watoto wachanga zaidi ya 120 na kinamama 25 jambo hili limetufurahisha sana tumeona ni muda muafaka kupeleka mradi huu katika mikoa mingine," alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na mafanikio hayo kuleta matokeo chanya wameweka utaratibu wa kuupeleka mradi wa kitita katika mikoa mingine minne ya Tanzania Bara.

Naye Mratibu wa Mpango wa Mradi wa Kitita cha Uzazi Salama, Mkoa wa Manyara, Beatrice Githiri, alisema wamekua wakitoa vifaa na mafunzo kwa wauguzi ili kuokoa maisha ya wajawazito na watoto.

Alisema mradi umesaidia kuboresha huduma kwa wateja na umepunguza vifo kwa kuwa awali hakukuwapo vifaa vya kutosha na utaalamu wa kutoa huduma hasa kutoa hewa kwa watoto ipasavyo baada ya kuzaliwa.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Babati, Renatha Herman, alisema mradi huo uko katika vituo sita na unajihusisha kuokoa vifo vya kinamama na watoto wachanga kabla na baada ya kujifungua.

Alisema: "Tangu kuanzishwa kwa mradi huu mwaka 2021 wanawake 7,421 wamepatiwa huduma za afya na watoto waliosaidiwa kupumua ni 127 kwa kuwa bila kuwapo kwa ujuzi na vifaa bora na vya kisasa wangeweza kupoteza maisha kwa kukosa msaada huo, pia vifo vya kinamama na watoto vimepungua."





# Mradi Ziwa Victoria wamaliza tatizo ukosefu maji kata mbili

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANANCHI wa Tinde na Didia wilayani Shinyanga waliokuwa wakinunua dumu la maji kwa Sh.500 na wakati mwingine kuchangia na mifugo, wameondokana na kadhia hiyo baada ya kuletewa mradi wa majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wananchi wa maeneo hayo walisema hali ya upatikanaji wa maji katika eneo hilo ulikuwa mgumu husus
ani wakati wa kiangazi, lakini kwa sasa baadhi ya wananchi wamefanikiwa kuvuta maji katika makazi yao.

Baadhi ya wakazi hao akiwamo Asha Hamadi, alisema awali walikuwa wakitumia maji yasiyofaa kutoka katika mabwawa na visima ambayo yalikuwa na chumvi, lakini sasa hivi wanatumia maji ya kutoka Ziwa Victoria ambayo ni salama kwa afya zao. Naye Paulo Bwire alisema kipindi cha nyuma kaba ya kuletewa kwa mradi huo, walikuwa wakiuziwa maji dumu moja Sh.500, lakini kwa sasa baadhi ya wananchi wamevuta maji kwenye makazi yao na hawana shida tena.

Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji Maji na Nishati (Ewura CCC) mkoani Shinyanga, Kudely Sokoine, akizungumza wakati wa ziara ya kamati hiyo kutembelea miradi ya maji ambayo imetekelezwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) katika Mji wa Tinde na Didia alionesha kuridhishwa na ubora wa utekelezaji wa miradi hiyo.

Alisema wamefarijika kuona miradi hiyo ya maji imetekelezwa kwa kiwango bora, pamoja na wananchi kupatiwa huduma stahiki ya maji.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Mhandisi Yusuph Katopola, alisema mamlaka hiyo itaendelea kuboresha utoaji wa huduma bora ya maji kwa wananchi.

Alibainisha kwamba katika Mji wa Didia, serikali imetoa Sh.milioni 700, kwa ajili ya kuongeza mtandao wa maji kutokana na kuwapo kwa Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), ambapo kumekuwapo na ongezeko la watu na kueleza kuwa katika mji huo hadi sasa wana wateja 400, Tinde wateja 200.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Bugomba 'A', Kata ya Ulewe, Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, baada ya kuzindua shule za msingi zilizojengwa kwa fedha za mradi wa boost wilayani humo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Walimu, mama lishe wapewa majiko, mitungi ya gesi bure

**Na Mwandishi Wetu,**
KAGERA

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, walimu, watumishi wa afya, mama lishe kutoka wilaya za Mkoa wa Kagera wamepewa mitungi ya gesi 300 na majiko bure.

Ugawaji wa mitungi huo uliratibiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera ukisimamiwa na Mkuu wa Mkoa huo, Fatma Mwasa.

Akizungumza wakati wa ugawaji mitungi hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwasa alisema msaada huo utawezesha wananchi wake kuendelea kutunza mazingira hasa miti ya asili.

Mwasa alisema ni vyema wananchi wa mkoa huo wakaendelea kutunza misitu kwa kutokata miti ovyo na njia ya kutunza misitu ni kutumia nishati safi ya kupikia ikiwamo gesi.

Alisema Serikali ya Mkoa wa Kagera imeendelea kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Aidha, aliipongeza Kampuni ya Oryx Gas Tanzania kwa kutoa mitungi ya gesi kwa wawakilishi wa makundi mbalimbali mkoani kwake.

"Nawashukuru kwa kuuangalia Mkoa wa Kagera lakini niendelee kuwasisitiza wananchi acheni kukata miti kwa ajili ya kuni na mkaa," alisema.

Alisema kuna faida kubwa ya kutumia nishati safi na salama ya kupikia kama gesi, kwanza kunakuwa na uhakika wa usalama wa afya kwa wananchi kwa sababu ya kutokuwapo kwa moshi.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Oryx Gas Tanzania, Araman Benoite, Antonia Kilama alisema lengo la kampuni hiyo kuunga mkononi jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akihimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Kampuni yetu tumekuwa tukiunga mkono juhudi za serikali ambayo imeweka lengo la kufikia asilimia 80 ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2030," alisema.

Meneja Masoko wa kampuni hiyo, Peter Ndomba alisema hadi sasa kampuni hiyo imeshatoa bure mitungi ya gesi na majiko 10, 000 katika mikoa mbalimbali nchini na hivyo kugusa makundi yote kwenye jamii.

# Wanne mbaroni tuhuma wizi wa saruji ya zahanati

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

JESHI la Polisi wilayani Sengerema mkoani Mwanza limewakamata watu wanne katika Kijiji cha Mayuya wakituhumiwa kuiba mifuko 15 ya saruji.

Akielezea tukio hilo Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mayuya, Shija Kasiani alisema watu hao walikamatwa baada ya msako wa kuwapata wahusika wa tukio la wizi wa mifuko 15 ya saruji iliyoibiwa katika ujenzi wa Zahanati ya Mayuya.

Aidha, Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Christina Masumbuko alisema kuwa baada ya mifuko hiyo kuibiwa kwa kushirikiana na polisi walianza kutafuta wahusika na ndipo walipokuta ikiwa imetelekezwa katika mashamba ya Shule ya Msingi Mayuya.

Akihojiwa kabla ya kukamatwa mlinzi wa vifaa vya ujenzi wa zahanati hiyo, Abeli Yohana ambaye pia ni miongoni mwa watuhumiwa alisema alingundua kuwa saruji hiyo iliibiwa baada ya kukuta mifuko hiyo imepungua na kuujulisha uongozi, huku watuhumiwa wengine wakikiri kuhusika na wizi huo.

Diwani wa Kata ya Tabaruka, Sospeter Busumabu, aliwaomba wazazi kuacha kuwakumbatia watoto wao wanaojihusisha na masuala ya wizi, huku akiwataka vijana kujishughulisha na kazi na kuachana na masuala ya wizi.

# Bil.6.7/- kupeleka maji Ushetu

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

SERIKALI kupitia Wizara ya Maji imetoa Sh. bilioni 6.7 katika mwaka wa fedha 2023/2024 ili kutatua tatizo sugu la ukosefu wa majisafi na salama lililodumu kwa muda mrefu katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi wa halmashauri hiyo walisema kutumia maji yasiyo safi na salama kutoka katika visima na mabwawa waliyoyachimba wao wenyewe, huku wakikabiliwa na tatizo la milipuko ya magonjwa inayotokana na matumizi ya maji yasiyo salama.

Paulina Julias Mkazi wa Ulewe alisema wakazi wenye visima katika makazi yao wanawauzia ndoo moja ya maji ya lita 20 kwa Sh. 1,000.

Alisema wananchi wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama hiyo wanalazimika kutumia maji kwenye mabwawa yaliyochimbwa kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

"Tunatumia maji haya kwa sababu hatuna namna, gharama za kuchimba kisima nyumbani ni kubwa sana na futi moja inachimbwa kwa Sh. 2,000 na ili upate maji unahitaji futi 20 hadi 25 kulingana na eneo lako, hivyo tunaomba mradi huo utekelezaji wake usichukue muda sana ili tupate maji," alisema Monica Maduhu mkazi wa Sabasabini.

Mkurugenzi wa Usambazaji Maji kutoka RUWASA, Mhandisi Mkama Bwire, aliwaeleza wakazi wa Kijiji cha Bugomba 'A' Kata ya Ulewe pamoja na Naibu Waziri OR-TAMISEMI, Deogratius Ndejembi, kuwa utekelezaji wake utanatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Alisema tayari wamemaliza kufanya utafiti na wamepata vibali vya kuanza utekelezaji wa mradi huo na wanatarajia kujenga tangi kubwa lenye ujazo wa lita 500,000 katika Kata ya Ulowa ambalo litasambaza maji katika kata zote.

Bwire alisema awali walilazimika kufanya utafiti na kuchimba visima virefu vya maji lakini hawakuweza kupata maji ya kutosha kama walivyotarajia licha baadhi ya maeneo kupatikana kwa huduma hiyo.

Hivyo aliwataka wananchi kuendelea kutumia maji katika visima hivyo, huku wakiendelea na utekelezaji wa mradi.

Naye Naibu Waziri OR-TAMISEMI, Deogratius Ndejembi, alisema, serikali imeendelea kutatua changamoto zinazowakabili wananchi katika sekta za afya, elimu, maji, kilimo na barabara.

Alisema atahakikisha anausimamia mradi huo kwa kushirikiana na Wizara ya Maji ili ukamilike kwa wakati na kuwahudumia wananchi.

Nipashe
Spotika



ADA 5 ZA JUU ZAIDI KWENYE USAJILI HUU 12 - 13



# WASHAMBULIAJI BORA WA EPL 2023/24

**LONDON, England**

LIGI Kuu ya England inaweza kuwa imempoteza Harry Kane msimu huu wa majira ya joto, lakini bado inajivunia baadhi ya washambuliaji bora kwenye sayari hii.

Iwe unataka mabao, pasi za mabao au kitu kingine chochote, unaweza kukipata kwenye Ligi Kuu kila wakati, huku magwiji na wapiga mipira ya adhabu ndogo wakihangaika mara kwa mara.

Hapa kuna viwango vya nguvu vya washambuliaji katika msimu wa 2023/24.

Hakuna mchezaji aliyeweza kupiga mashuti mengi yaliyolenga lango katika raundi ya kwanza ya mechi za msimu huu kama Callum Wilson, ambaye anaendelea kupendeza katika maisha yake kule Newcastle kwenye Uwanja wa St James' Park.

Hapa tunawaangalia washambuliaji wa kiwango cha juu zaidi kwenye Ligi Kuu England...

**#9. Ollie Watkins**

Aston Villa walikuwa wabaya dhidi ya Newcastle United kwenye mechi yao ya ufunguzi, lakini haikuwa kwa kukosa kujaribu kutoka kwa Ollie Watkins.

Wakiwa wamechangamka tena chini ya kocha Unai Emery, Watkins alicheza vema kwa muda wote na kuweka bao pekee la Villa katika mchezo huo. Hatuhitaji tu kuzungumza juu ya kile kilichotokea baadaye.

**#8. Matheus Cunha**

Huenda Matheus Cunha hajafunga bao dhidi ya Manchester United, lakini alituma ujumbe mzito kwa wachezaji wengine wote wa Ligi Kuu England kwa kiwango kikubwa.

Siku nyingine, Cunha anaweza kuwa na mabao machache kwa jina lake. Si mbaya kwa mchezaji ambaye wengi walikuwa wakienda mbali wakati anajiunga na Wolves.

**#7. Jarrod Bowen**

Akiwa na matokeo mazuri katika sare ya bao 1-1 kati ya West Ham na Bournemouth, Jarrod Bowen anatafuta vita ya kurudisha timu yake kwenye ubora wao.

Bowen alishinda bao bora la mwezi na atatumaini kuendeleza kasi hiyo.

**#6. Kaoru Mitoma**

Kaoru Mitoma anaweza kuwa winga bora zaidi wa mmoja-mmoja kwenye Ligi Kuu kwa sasa.

Mchawi huyo wa Brighton alikuwa hapo tena wikendi iliyopita aliposaidia kuwakaribisha wageni wapya, Luton Town.

**#5. Luis Diaz**

Mchezaji mkali katika mechi za kujiandaa na msimu mpya, Luis Diaz, aliendelea na kiwango hicho hadi mechi ya kwanza ya Liverpool dhidi ya Chelsea, akifunga bao pekee la timu yake.

Kwa hakika mechi za kirafiki hazihesabiki, lakini Diaz amefunga kiufundi katika mechi zake tatu zilizopita. Hebu tuone hiyo itachukua muda gani.

**#4. Harvey Barnes**

Kutakuwa na usajili wa kuvutia zaidi msimu huu wa majira ya joto kuliko uhamisho wa Harvey Barnes wa pauni milioni 39 kwenda Newcastle, lakini wachache watakuwa na ufanisi kama huo.

Barnes alicheza papo hapo katika klabu yake mpya, akitokea benchi na kufunga bao na kutoa pasi za mabao.

**#3. Bukayo Saka**

Huhitaji kuambiwa kwamba Bukayo Saka ni mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu. Ni maarifa ya kawaida siku hizi.

Nyota huyo wa Arsenal msimu huu alianza, akishinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Mechi baada ya kufunga bao katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Nottingham Forest.

**#2. Alexander Isak**

Ubora wa Newcastle United na utajiri katika mashambulizi unaendelea.

'The Magpies' walipata ushindi mnono zaidi wa raundi hiyo na hilo linatokana na Alexander Isak, ambaye alifunga mara mbili dhidi ya Villa.

**#1. Erling Haaland**

Erling Haaland alihitaji dakika nne tu za msimu kutukumbusha sote kile anachofanya vizuri, na alikuwa mshindi wa Manchester City dhidi ya Burnley kwa mabao mawili kwa jina lake. Je, rekodi yake mwenyewe iko hatarini? Tusubiri kuona tena.

## ISIKUPITE

Lionel Messi amefunga bao lake la 10 katika mechi saba alizoichezea Inter Miami ya Marekani, na kuiwezesha kutwaa Kombe la Ligi baada ya jana kuiongoza timu hiyo kushinda mechi ya fainali kwa mikwaju ya penalti 10-9 dhidi ya Nashville SC hatua hiyo ikifikiwa baada ya dakika 90 za mchezo kumalizika kwa sare ya bao 1-1. Kombe hilo ni la kwanza kwa Inter Miami tangu ilipoanzishwa mwaka 2020.



## Extra Time

# ADA 5 ZA JUU ZAIDI KWENYE USAJILI HUU



Moises Caicedo

**LONDON, England**

SIKU zimepita ambapo mikataba ya uhamisho yenye thamani ya euro milioni 100 ilikuwa adimu. Sasa ni jambo la kawaida, haswa linapokuja suala la wanasoka bora ambao bado wana miaka mingi iliyobaki kucheza.

Soko la uhamisho limeongezeka na imekuwa kawaida kwa timu kudai fedha nyingi kwa wachezaji wao wakuu. Mikataba kadhaa ya uhamisho iliyothibitishwa na kuripotiwa msimu huu wa majira ya joto ni uthibitisho wa hili.

Msimu huu wa majira ya joto, tumeona ongezeko kubwa la mikataba ya fedha nyingi. Huku kukiwa bado na muda mwingi kwenye dirisha la uhamisho wa wachezaji, bado tunaweza kuona klabu nyingi zikivunja benki ili kupata huduma za wachezaji zinazowatamani.

Makala haya yameangalia ada tano za uhamisho zilizoripotiwa kutoka kwenye dirisha hili la uhamisho ambazo ni za juu zaidi...

**#5 Malcom - Euro Milioni 60**

Al-Hilal ni moja ya Klabu ya Saudi Aarabia ambayo imeonesha nia kubwa katika soko la usajili msimu huu wa majira ya joto. Wamewasajili wachezaji kama Kalidou Koulibaly, Sergej Milinkovic-Savic, Ruben Neves na Malcom katika miezi michache iliyopita.

Malcon amegharimu euro milioni 60. Kusema ukweli, winga huyo wa Brazil alikuwa na kampeni nzuri sana ya 2022-23 kule Zenit St. Petersburg. Alifunga mabao 26 na kutoa pasi tisa za mabao kwenye mechi 33 katika mashindano yote.

Lakini tofauti na wachezaji wengine mashuhuri ambao wamehamia Al-Hilal muhula huu, Malcom hakuwa akichezea kwenye klabu ambayo ipo kwenye Ligi Kuu tano bora za Ulaya.

**#4 Kai Havertz - Euro Milioni 75**

Chelsea ilimsajili Kai Havertz kutoka Bayer Leverkusen msimu wa majira ya joto wa 2020 kwa kitita cha euro milioni 80. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani alikuwa na matukio machache ya kukumbukwa akiwa na jezi ya Chelsea.

Hata hivyo, hakuwahi kufikia kilele kilichotarajiwa kwake katika kipindi cha misimu mitatu aliyocheza Stamford Bridge. Makubaliano kati ya mashabiki na wachambuzi yanaonekana kuwa hakuweza kuhalalisha bei yake wakati akiwa klabuni hapo.

Kwa ujumla, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alifunga mabao 32 na kutoa asisti 15 katika mechi 139 kwenye michuano yote aliyoichezea Chelsea. Lakini licha ya kutokuwa na msimu mzuri kule Stamford Bridge, 'The Blues' waliweza kurejesha karibu kiasi chote walicholipa kupata kwa huduma yake miaka mitatu nyuma.

Yeye si mshambuliaji wa kati na tayari wana wachezaji wazuri wa kati wa kushambulia kwenye malipo yao.

**#3 Rasmus Hojlund - Euro Milioni 75**

Ni kweli kwamba Manchester United ilihitaji kuwekeza kwa mshambuliaji mchanga wa kati ambaye anaweza kuwa kwenye jezi hiyo kwa muda mrefu. Lakini licha ya kipaji kikubwa alichotoa katika msimu wa 2022-23, Rasmus Hojlund ni mchezaji ambaye bado hajathibitishwa na kuna uhakika mdogo wa kufanikiwa Old Trafford.

Alifunga mabao tisa pekee na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 32 za Serie A msimu uliopita. Kutoa kiasi cha euro milioni 75 kwa mchezaji kunaweza kuwa kama mchezo wa kubahatisha.

**#2 Lucas Paqueta - Euro Milioni 81**

Lucas Paqueta alijiunga na West Ham United kutoka Lyon kwa dili la euro milioni 42 msimu uliopita. Alifunga mabao matano na kutoa asisti saba katika mechi 41 katika mashindano yote kwa 'Wagonga Nyundo' hao msimu uliopita. Ana miaka miwili zaidi katika mkataba wake wa sasa na West Ham na hawana nia ya kumuuza hivi sasa.

Manchester City waliripotiwa kuweka mezani dau la euro milioni 81 kwa ajili ya kiungo huyo wa kati wa Brazil wiki iliyopita. Ingawa yeye ni mchezaji bora, akiwa na Euro milioni 81, Paqueta bila shaka ni ghali zaidi.

Lakini hata kiasi hicho kikubwa huenda kisiipate City, mchezaji huyo kwani West Ham wameripotiwa kukataa ombi lao na wanataka zaidi.

Wakati City hawana uhaba wa fedha za kulipa, wanapaswa kuwa waangalifu na historia wanayoweka kwa kuvunja benki ili kusajili mchezaji ambaye anaweza asiboresha sana timu yao.

**#1 Moises Caicedo - Euro milioni 133**

Moises Caicedo ameripotiwa kukataa nafasi ya kwenda Liverpool baada ya 'Wekundu' hao kukubaliana ada na Brighton & Hove Albion kwa huduma yake siku chache zilizopita. Kiungo huyo mchanga amejiunga na Chelsea ambayo ilikuwa ikimwania kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa Sky Sports, Chelsea wamelipa kitita cha euro milioni 133 kumnunua kiungo huyo wa Ecuador. Caicedo bila shaka ni mmoja wa viungo bora zaidi wa ulinzi kwenye Ligi Kuu England na ameweka historia ya usajili ghali zaidi katika historia ya ligi hiyo.


Hicho ni kiasi cha fedha cha kuchukiza kutumia kwa kiungo mkabaji. Ili kuweka mambo sawa, wachezaji kama Declan Rice na Rodri wote wana thamani ya euro milioni 90.

## Nukuu


"Nadhani Manchester United ndio Spurs wapya. Wamekata tamaa. Tusi kubwa zaidi...huwa nafikiria kuhusu timu ambazo haziwezi kufanya hivyo ugenini au wachezaji ambao hawako tayari kwa hilo ugenini. Wao ni timu nzuri, wanatamani wakati mashabiki wao wa nyumbani wako mbele yao. Wanapata msaada huo na nguvu," **Kiungo wa zamani wa Manchester United, Roy Keane, akiichambua timu hiyo baada ya kutoridhishwa na kuiona ikiangukia kipigo cha mabao 2-0 ugenini dhidi ya Tottenham, juzi.**



"Nisingeweza kuketi hapa ikiwa tungetumia kile ambacho Chelsea alikitumia katika madirisha mawili ya mwisho ya usajili - ungeniua. Mtaniua, hilo ni hakika, tungekuwa chini ya uchunguzi kama vile usingeweza kufikiri. Tunapaswa kuona kile kinachotokea sokoni na ikiwa tunaweza kufanya hivyo na kulipa kile tunachoamini kuwa ni haki," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola akipigilia msumari kwa vyombo vya habari akidai 'wangemuua' endapo angetumia pesa nyingi sokani kama Chelsea mwaka uliopita.**



"Kazi yangu ni kuwa mwadilifu kwa kila mtu kwenye kikosi. Kusajili mchezaji kwa mkataba wa miaka minane na kama hatahusika, hakuna kujituma, hatacheza. Kama hawataki kupigania nafasi yao na kuhisi ni sehemu ya timu kucheza au kutocheza, mlango uko wazi. Ikiwa wachezaji wana wazo wazi kwamba wanahitaji kushindana kwa nafasi yao na ni makocha wanaoamua kwa kila mchezo, ni rahisi," **Kocha wa Chelsea, Mauricio Pochettino akielezea nia yake ya kuwaruhusu wachezaji kuondoka endapo hawatakuwa na furaha hapo Stamford Bridge.**





Kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto'.**PICHA: AZAM**

# MAMBO 10 USIYOYAJUA MECHI ZA MWANZO LIGI KUU 2023/24

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24, ilianza Jumanne iliyopita kwa timu kadhaa kuanza mbio za kulisaka taji ya ubingwa.

Kama ilivyotarajiwa ligi imeanza kwa kishindo, ugumu na matokeo yaliyotarajiwa na yasiyotarajiwa pia huku timu nyingi zikionekana kujizatiti kisawasawa.

Katika makala haya tumekusanya taarifa, takwimu na rekodi za mechi za ufunguzi wa Ligi Kuu na moja ya raundi ya pili iliyochezwa juzi kati ya Namungo na KMC.

Takwimu na rekodi hizi zimewekwa na wachezaji pamoja na timu zenyewe za Ligi Kuu, twende sasa...

**#1. Simba haijapoteza misimu 16**

Ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Mtibwa Sugar, unaifanya Simba kutopoteza mechi yoyote ya ufunguzi kwa misimu 16 mfululizo. Mara ya mwisho ilipoteza msimu wa 2007/08 ilipochapwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga dhidi ya Coastal Union ambalo liliwekwa wavuni dakika ya 44 na Sunday Peter.

Katika mechi hizo, Simba imeshinda 13 na kutoka sare tatu. Ulikuwa msimu wa 2013/14 ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Rhino Ranger, uliofuata ilitoka sare kwa mara nyingine tena ya mabao 2-2 dhidi ya Coastal Union na msimu wa 2021/22 ilisuluhu dhidi ya Biashara United.

**#2. Yashindwa kuweka rekodi ya 2017/18**

Pamoja na kushinda idadi hiyo ya mabao, Simba imeshindwa kuweka rekodi iliyoiweka msimu wa 2017/18 ilipoichakaza Ruvu Shooting mabao 7-0 Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Emmanuel Okwi akipachika manne, Shiza Kichuya, Juma Luzio na Erasto Nyoni wakifunga bao moja kila mmoja.

Mara ya mwisho timu hiyo kufunga mabao manne kwenye mechi ya ufunguzi kama ilivyofanya dhidi ya Mtibwa Sugar ilikuwa msimu wa 2008/09 ilipoiadhibu Villa Squad mabao 4-1, mawili yakifungwa na Mnigeria Emeh Izuchukwu, Mussa Hassan Mgosi na Ramadhani Chombo 'Redondo', wakifunga bao moja kila mmoja.

**#3. Mapro watawala ufungaji**

Kwa misimu miwili mfululizo, mabao yote ya mechi zake za kwanza yanafungwa na wachezaji wa kigeni.

Msimu uliopita ilipoifunga Geita Gold mabao 3-0 kwenye mechi ya ufunguzi, mabao yalifungwa na Wazambia Clatous Chama na Moses Phiri, lingine likiwekwa kwenye kamba na Mghana ambaye kwa sasa hayupo kwenye kikosi, Augustine Okrah.

Msimu huu yamefungwa na Wakongomani Jean Baleke na Fabrice Ngoma, Mzambia Chama akiingia tena kwenye rekodi ya kuwa katika orodha ya wafungaji wa mabao ya raundi ya kwanza pamoja na Mcameroon, Willy Onana.

Mara ya mwisho Wabongo kufunga mabao kwenye mechi ya ufunguzi kwa timu hiyo ilikuwa msimu wa 2020/21 ilipoifunga Ihefu 2-1, yakitumbukiwa nyavuni na John Bocco na Mzamiru Yassin.

**#4. Azam haijapoteza tangu 2009**

Azam FC ilianza Ligi Kuu msimu huu kwa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Kitayosce Jumatano iliyopita katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, ikiweka rekodi ya kutopoteza mechi yoyote ya ufunguzi kwa misimu 14.

Katika mechi hizo, imeshinda 10 na minne ikitoka sare msimu wa 2013/14 ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, 2016/17 sare tena ya bao 1-1 dhidi ya African Lyon, suluhu dhidi ya Simba msimu wa 2017/18 na 2021/22 dhidi ya Coastal Union sare ya bao 1-1.

Azam haijapoteza mechi yoyote ya kwanza tangu ilipofungwa mabao 3-2 mechi ya ufunguzi Agosti 23, 2009, msimu wa 2009/10 kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera. Yalikuwa ni mabao ya Paul Kabange, Michael Katende na Themi Felix, John Bocco akiifungia Azam mabao mawili.

**#5. Dube kama Chama**

Wakati Chama wa Simba akifunga bao kwenye mechi ya kwanza kwa misimu miwili mfululizo, Prince Dube ameweka kama hiyo. Dube amefunga bao moja katika mechi ya ufunguzi dhidi ya Kitayosce msimu huu, alifanya hivyo pia msimu uliopita, Azam ikiichapa Kagera Sugar mabao 2-1, lingine likifungwa na Tepsi Evance, Anuary Jabir akiifungia timu yake bao la kufutia machozi.

**#6. Fei Toto aweka rekodi ya 'hat-trick'**

Kiungo wa Azam FC, Feisal Salum, ameweka rekodi ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' ndani ya dakika 13 tu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu yake dhidi ya Kitayosce, timu yake ikishinda 4-0. Ilikuwa ni hat-trick ya kwanza msimu huu kwenye mechi ya kwanza pia ya Ligi Kuu.

Ni hat-trick ya mapema zaidi kwenye historia ya Ligi Kuu, akivunja rekodi iliyowekwa ya straika wa Simba, Jean Baleke, aliyoiweka msimu uliopita, Machi 11, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro ilipocheza dhidi ya Mtibwa Sugar timu yake ikishinda mabao 3-0. Baleke alifunga dakika ya tatu, saba na 34, wakati Fei Toto alifunga dakika ya tatu, tisa na 13.

**#7. Ihefu kama msimu uliopita**

Ihefu ilianza mechi ya kwanza nyumbani kama ilivyokuwa msimu uliopita na ikapoteza kwa bao 1-0 kwa mara nyingine tena, tarehe ikiwa ile ile na uwanja ule ule, Highland Estates, Mbarali.

Jumanne iliyopita, Agosti 15 ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Geita Gold, likiwekwa wavuni na Elius Maguri. Ilikuwa kama 'kukopi' na 'kupesti' kwa matokeo ya ufunguzi msimu uliopita ilipodunguliwa bao 1-0, Agosti 15, mwaka jana likiwekwa wavuni na Ally Bilal.

**#8. Kagera yapoteza mbili tena**

Kama msimu uliopita, timu ya Kagera Sugar imepoteza mechi mbili za kwanza msimu huu.

Ilianza kupoteza Jumatano iliyopita ugenini dhidi ya Mashujaa FC kwa mabao 2-0, kabla ya Jumamosi kufunga bao 1-0 dhidi ya Uhefu FC.

Imerudia rekodi mbaya ya msimu uliopita ilipopoteza mechi ya ufunguzi kwa kulala mabao 2-1 dhidi ya Azam FC, kabla ya kubamizwa 2-0 dhidi ya Simba.

**#9. Namungo sare misimu miwili**

Tangu iliposhinda mabao 2-0 msimu wa 2021/22, timu ya Namungo haijashinda mechi yoyote ya ufunguzi kwa misimu miwili mfululizo, badala yake imetoka sare zote.

Juzi ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi ikirudia ilichokifanya mechi ya ufunguzi msimu uliopita ilipotoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mtibwa Sugar, Septemba 27, 2021, Ligi Kuu msimu wa 2021/22.

**#10. Mashujaa kama Singida FG**

Ushindi wa mabao 2-0 ilioupata Mashujaa FC dhidi ya Kagera Sugar Jumanne iliyopita, umeweka rekodi ya misimu miwili mfululizo kwa timu moja inayopanda daraja kushinda mechi ya ufunguzi.

Msimu uliopita, Singida Fountain Gate ilikuwa timu pekee iliyopanda daraja kushinda mechi ya ufunguzi kwa kuifunga Prisons bao 1-0, Agosti 16, mwaka jana.

**JE, WAJUA?**



KOCHA Robertinho Oliveira hajawahi kupokea kipigo kwenye Ligi Kuu Bara tangu atue kuiongoza Simba, haya ndio matokeo aliyoyapata:- Simba 3 -2 Mbeya City, Dodoma Jiji 0 - 1 Simba, Simba 3-1 Singida Big Stars, Simba 1- 1 Azam FC, Mtibwa Sugar 0 - 3 Simba, Simba 6 - 1 Prisons, Ihefu 0 - 2 Simba, Simba 2 - 0 Yanga, Namungo 1 -1 Simba, Simba 3 - 0 Ruvu Shooting, Simba 6 - 1 Polisi Tanzania, Simba 3 - 1 Coastal Union, Mtibwa Sugar 2 - 4 Simba.



## HABARI DODOMA

# Chanzo kupaa makusanyo katika madini chatajwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

USIMAMIZI mzuri ulipo hivi sasa katika sekta ya madini nchini umetajwa kuwa moja ya sababu kuu ya kuchangia kasi ya ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli na utoaji wa leseni kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Mhandisi Ramadhani Lwamo, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema kuwa kiwango cha makusanyo ya maduhuli ya serikali kilipanda kutoka Sh. bilioni 624.61 zilizokusanywa mwaka 2021/2022 na kufikia Sh. bilioni 678.04 mwaka wa fedha 2022/2023, makusanyo haya ni sawa na asilimia 82.49 ya lengo la mwaka ambalo lilikuwa ni Sh.bilioni 822.

Alibainisha kwa kipindi hicho Tume ya Madini ilifanikiwa kutoa jumla ya leseni za madini 9,642 kati ya leseni 9,174 zilizopangwa kutolewa zikiwamo leseni za uchimbaji mkubwa, uchimbaji wa kati, uchimbaji mdogo, biashara ya madini pamoja na uchenjuaji wa madini.

Aidha, alisema kati ya leseni zilizotolewa, leseni 6,511 sawa na asilimia 70.97 zilitolewa kwa wachimbaji wadogo ikiwa ni mkakati wa serikali ya awamu ya sita katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuongeza mchango wao katika sekta ya madini.

Kuhusu hali ya masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini, Mhandisi Lwamo alisema serikali imeanzisha masoko ya madini 42 na vituo vidogo vya ununuzi wa madini 94 nchini.

Alisema kuwa kwa kipindi hicho masoko na vituo vya ununuzi wa madini vilichangia jumla ya Sh. bilioni 157.4 kama mrabaha na ada ya ukaguzi wa madini nchini ikiwa ni sawa na asilimia 23.22 ya makusanyo yote yaliyokusanywa na Tume ya Madini katika mwaka husika.

Alisema: "Ukuaji wa sekta ya madini umeongezeka kutoka asilimia 9.6 mwaka 2021 hadi 10.9 mwaka 2022. Tunaamini tutaweza kufikia mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa wa asilimia 10 au zaidi ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoelekezwa katika ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 na Dira ya Maendeleo ya Taifa".




Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Lugano Wilson (katikati), akikata utepe kuzindua mtambo wa kusafisha mafuta ya alizeti kiwanda cha Quickstep Investment Ltd, katika kijiji cha Mkoka wilayani Kongwa mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki. Mtambo huo, wenye thamani ya Sh. milioni 17.9 umetolewa msaada na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO). **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yapewa dawa kutokomeza ajali zembe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuweka mikakati ya kukomesha ajali nchini ikiwamo mafunzo maalum ya mara kwa mara kwa madereva wa serikali ambao wamekuwa wakilalamikiwa kutozingatia sheria za usalama barabarani.

Mkuu wa Chuo cha Mafunzo ya udereva cha Wide jijini Dodoma, Faustine Matina, alitoa ushauri huo jana kwenye mafunzo kwa madereva wa malori wasiokuwa na vyeti vya udereva ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Jeshi la Polisi.

Alisema madereva hao wamekuwa wakilalamikiwa kuendesha kwa mwendokasi na kutofuata sheria hiyo na kushauri serikali kuwakumbusha wajibu wao ili kuepuka ajali ambazo zinaligharimu taifa.

"Kazi ya vyuo vya udereva ni kuhahakikisha kuwa tunaandaa madereva bora ili kukabiliana na tatizo la ajali za barabarani kutokana na uzembe hapa leo tunao madereva wa malori ambao wanaleseni lakini hawana mafunzo ya udereva tunawafundisha sheria za usalama barabarani, utii wa sheria bila shuruti kuwa watiifu wanapokuwa njiani na vyombo vya moto," alisema.

Alisema kuna umuhimu wa mafunzo hayo kuwa endelevu ili kukomesha ajali za barabarani zinazotokana na makosa ya kibinadamu.

"Serikali iandae utaratibu maalum kwa ajili ya madereva wa serikali ambao wamekuwa wakilalamikiwa namna wanavyoendesha vyombo vyao hawazingatii sheria za usalama barabarani," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Madereva wa Tipa Dodoma (UMATIDO), Praygod Malle, alikishukuru chuo hicho kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kutoa mafunzo hayo.

"Tunaishukuru serikali yetu kwa kutoa maagizo ambayo yamewezesha leo madereva kupata mafunzo ambayo yatakwenda kupunguza tatizo la ajali nchini ambazo nyingi zimekuwa zikitokea kwa makosa ya kibinadamu," alisema.

Hata hivyo, alitoa wito kwa madereva wote ambao wanaendesha vyombo vya moto bila kuwa na mafunzo kuchangamkia fursa hiyo ili kuepuka kusumbuliwa na mamlaka katika operesheni mbalimbali za ukaguzi wa leseni.

# 'Kupunguza, kufutwa tozo za OSHA kutavutia wawekezaji'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema kupunguzwa na kufutwa baadhi ya tozo zilizokuwa zikitozwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) za Sh.bilioni 35 inalenga kuweka mazingira mazuri ya wawekezaji nchini.

Katambi alibainisha hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ilipokuwa ikipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu na mafanikio ya OSHA.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliliridhia ombi la wafanyabiashara kupitia Chama Cha Waajiri Tanzania (ATE) kuhusu tozo hizo hali ambayo imeendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini.

Alisema masuala ya usalama na afya mahali pa kazi yataendelea kupewa uzito na serikali ili kuhakikisha nguvu kazi iliyopo inakuwa salama.

Naye Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema tozo ya upimaji umeme katika vituo vya mafuta hasa maeneo ya vijijini imepunguzwa kutoka Sh.650,000 hadi Sh.150,000 ili kuvutia wawekezaji na kuondokana na mafuta kuuzwa kwenye chupa.

Alisema kumekuwapo na matokeo chanja ambapo OSHA imevifikia vituo 2,708 ikilinganishwa na kabla ya kupunguzwa tozo vilifikiwa vituo 1,153.

Kadhalika, alisema kutokana na Tanzania kutekeleza kwa kiwango kikubwa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi imekuwa mfano kwa mataifa mengine kuja kujifunza.

Akihitimisha kikao cha kamati hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq alipongeza serikali kwa kuendelea kufanyia kazi maoni ya kamati ya kuimarisha masuala ya usalama mahali pa kazi kwa kuipatia OSHA vitendea kazi ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

# Serikali, Bunge wajadili kutokomeza malaria ifikapo 2030

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Afya na Kamati ya Bunge ya Afya, imekutana kujadili afua za kutokomeza ugonjwa wa malaria ifikapo mwaka 2030 ili kuendelea kuimarisha sekta ya afya nchini.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha siku mbili chenye lengo la kujenga uwezo kwa wabunge na wajumbe wa baraza la kutokomeza maralia.

Alisema serikali, Bunge na wadau wanapaswa kuweka nguvu kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030 ili kuboresha afya za Watanzania.

Naye Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alilitaka baraza hilo kusimamia vyema rasilimali zilizopo za kutokomeza maralia ili kufikia malengo ya kuutokomeza ugonjwa huo.

Awali Mwenyekiti wa baraza hilo, Leodegar Tenga, alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika kupunguza idadi ya wagonjwa na vifo vitokanavyo na ugonjwa wa malaria.





## Viongozi wa CCM waagizwa kutoa somo 'R' nne za Samia

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

VIONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Mbeya, wameagizwa kuhakikisha wanawafafanuliwa wanachama wa chama hicho 'r' nne ambazo Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akizihubiri kila siku kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho (NEC) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela alitoa agizo hilo wishoni mwa wiki wilayani Rungwe alipokuwa anafungua mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa chama wa kata zote za wilaya hiyo.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Idara ya Uenezi ya Wilaya ya chama hicho kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi hao katika kukitumikia chama hasa kukijenga uanzia ngazi ya shina.

Mwaselela alizitaja 'r' hizo kuwa ni reconciliation (maridhiano), reform (mabadiliko), resilience (ustahimilivu) na re-building (kujenga upya) na kwamba ni msingi mkubwa wa amani na maendeleo ya taifa lakini wananchi wengi hawajui.

Alisema 'r' hizo zinatakiwa kuhubiriwa na kiongozi wa ngazi yoyote ya chama hicho pamoja na kuzitekeleza ili kujenga amani miongoni mwa wananchi wa maeneo yao

"Hizi r nne ni muhimu sana kwetu sote kwa hiyo nitumie hadhara hii kuwaagiza viongozi wa chama katika ngazi zote kuhakikisha wanazihubiri kwa wanachama, alipozisema rais ilikuwa tayari ni agizo kwahiyo kinachotakiwa ni utekelezaji tu," alisema Mwaselela.

Aidha aliupongeza uongozi wa CCM Wilaya ya Rungwe kwa kuanzisha mafunzo ya uongozi wa viongozi wa chama hicho ngazi ya kata akisisitiza kuwa viongozi wa wilaya zingine wanatakiwa kuiga ili kuboresha utendaji wao hasa katika kukijenga chama.

Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Rungwe, Osward Ambokile, alisema wameanzisha mafunzo hayo kwa ajili ya kuwajengea uwezo viongozi hao kwa maelezo kuwa baadhi yao hawana uzoefu kwenye uongozi kutokana na kutofundishwa.

# Vyama 14 kuchuana ubunge Jimbo la Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

VYAMA vya siasa 14 vinatarajiwa kuchuana kwenye uchaguzi mdogo wa ubunge Mbarali mkoani Mbeya ambao unatarajiwa kufanyika Septemba 19, mwaka huu.

Uchaguzi huo unafanyika kwa lengo la kuziba nafasi ya aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Francis Mtega ambaye alifariki hivi karibuni kwa ajali ya kugongwa na trekta dogo aina ya power tiller wakati akiendesha pikipiki kuelekea shambani.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa jimbo hilo, Misana Kwangula, alisema mchakato wa uchaguzi huo ulianza ndani ya vyama vya siasa baada ya tume kutangaza nafasi hiyo.

Alisema vyama vyote viliteua wagombe kwa kufuata taratibu za ndani ya chama na kisha wagombea wote wa vyama 14 wakachukua fomu katika ofisi yake na kuzirejesha kwa ajili ya taratibu za uteuzi isipokuwa mgombea wa chama kimoja pekee ndiye hakurejesha fomu hiyo.

Alivitaja vyama vinavyoshiriki uchaguzi huo kuwa ni Chama Cha Mapinduzi (CCM), Tanzania Labor Party (TLP), United Democratic Party (UDP), ACT-Wazalendo, Democratic Party (DP), AAFP, CCK, ADC, NLD, NRA, UMD, ADA TADEA, na Chama Makini.

"Fomu zilianza kutolewa Agosti 13 na mwisho ilikuwa Agosti 19, mpaka leo (Jumamosi) ambayo ndiyo siku ya mwisho kuchukua na kurejesha fomu, wagombea wa vyama vyote wamerejesha fomu isipokuwa mgombea wa chama kimoja pekee ambacho ni NRA," alisema Kwangula.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kurejesha fomu baadhi ya wagombea wa vyama hivyo kila mmoja alijinadi kuwa ataibuka na ushindi kwenye kinyang'anyiro hicho.

Mgombea wa CCM, Bahati Ndingo ambaye alikuwa Mbunge wa Viti Maalumu wa chama hicho kupitia Jumuiya ya Wazazi Taifa, alisema ana matumaini ya kushinda kwenye uchaguzi huo kutokana na kuungwa mkono na chama chake.

Alisema atafanya kampeni za kisasa na za kistaarabu ili kuhakikisha anashinda nafasi hiyo na kuanza kuwatumikia wananchi wa jimbo hilo kwa kuhakikisha anatetea haki zao.

"Chama changu kinaniunga mkono kwa nguvu sana kwahiyo nina imani kwamba tutashinda, nitafanya kampeni za kuomba kura nyumba kwa nyumba nikieleza mambo mazuri ambayo serikali ya CCM imewafanyia na ninaamini wananchi wataniunga mkono," alisema Bahati.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbarali, Mary Mbwilo ambaye aligombea nafasi hiyo kwenye kura za maoni alisema chama hicho kimepata mwakilishi makini ambaye wana uhakika ataipeperusha vizuri bendera ya chama hicho.

Mgombea wa Chama cha ACT -Wazalendo, Modestus Kilufi, ambaye aliwahi kuwa mbunge wa jimbo hilo kupitia CCM kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 alijinadi kuwa ataibuka na ushindi kwenye uchaguzi huo.

Kilufi alisema bado ana kiu ya kuwaongoza wananchi wa Mbarali hasa katika kupigania haki zao kwa maelezo kuwa wananchi wa wilaya hiyo wanakabiliwa na matatizo mengi ambayo bado hayajatatuliwa.

"Kwa muda mrefu tumekuwa tukihangaika na mipaka ya Hifadhi ya Taifa, kero za maji, migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikitusumbua kwa muda mrefu sana, ni wakati sasa tukipata ridhaa ya wananchi kwenda kushughulikia kero hizo," alisema Kilufi.

Wagombea wengine waliochukua na kurejesha fomu ni Hussein Msea wa ADA TADEA, Halima Magambo wa AAFP, Fatuma Rashid Zania wa NLD, Moris Ngonolo wa TLP, Bariki Manyalu wa Demokrasia Makini na Hashimu Abas wa ADC.

Hata hivyo Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeshatuma maofisa wake wilayani Mbarali kwa lengo la kutoa elimu kuhusu taratibu za uchaguzi huo ikiwamo gharama.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela (kushoto), akikabidhiwa simu 26 kwa Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya kusajilia wanachama wa chama hicho kwenye kata zote za wilaya hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanafunzi waonywa kujiingiza vitendo ukiukwaji maadili

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MDHIBITI Ubora wa Elimu Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Marry Msongolwa, amewaonya wanafunzi mkoani Njombe kutojiingiza kwenye vitendo vya ukiukwaji wa maadili vitakavyo wasababishia kufukuzwa shule na kuharibu maisha yao.

Msongolwa alitoa onyo hilo wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mtwango iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, wakati Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alipotembelea shuleni hapo.

Alisema mwanafunzi yeyote ambaye atabainika kufanya vitendo ambavyo ni kinyume na maadili ya kitanzania atachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Hapa mmetoka sehemu mbalimbali, mtu mwingine anasema katoka Katavi, mwingine amesema anatoka Iringa na wengine Dodoma sasa mnapokuta hapa na huo mchanganyiko kila mtu kule amejifunza mambo tofauti sasa nyinyi msije kubali mtu ametoka huko na mambo yake halafu anaanza kuwafundisha bwenini namna ya kuishi anawaletea maisha ambayo yanakwenda nje ya maadiili ya Watanzania," alisema Msongolwa. Msongolwa aliongeza kuwa: "Mtu anaanza kuwaambia awafundishe kufanya mapenzi ya jinsia moja na hata jinsia tofauti nyinyi bado ni wanafunzi sio wakati wenu".

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alisema anataka kuona wanafunzi wote katika mkoa wake wanasoma huku wakizingatia maadili mema na kwamba suala la nidhamu ndilo litakalo wafikisha kwenye mafanikio.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Christopher Sanga, aliahidi kutoa zawadi kwa wanafunzi watakaofanya vizuri katika mitihani yao ikiwa ni motisha ya juhudi zao katika masomo.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo, Gladness Mgaya na Jackson Elia waliomba serikali kuendelea kuwasaidia kutatua changamoto zinazowakabili shuleni hapo ikiwemo ukosefu wa majisafi.





SIAH MALLE

# Safari yake katika uhandisi inavyoibua vipaji vipya wanawake wenye ndoto

**Na Maria Seme, aliyekuwa**
ZANZIBAR

SIAH Malle ni mfano wa wanamke waliofanikiwa kuvunja dhana iliyojengeka na kuwagawa wanawake na wanaume kwenye uwanja wa taaluma.

Safari yake ya kuwa jaji katika Kongamano na Maonesho ya 8 ya Wanawake Wahandisi Tanzania (TAWECE) ni uthibitisho tosha kuwa ari na bidii yake katika tasnia ya uhandisi imezidi kumwinua.

Alipokuwa anakua, Siah alivutiwa na ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Kaka yake ambaye ni mhandisi wa ujenzi, alichochea shauku yake kuingia katika tasnia ya uhandisi na alidhamiria kufuata nyayo zake.

Vilevile, kwa kutiwa moyo na walimu wake, alisoma Sayansi na Hisabati katika elimu ya sekondari na kufanikiwa kufaulu vizuri masomo hayo.

Baadaye Siah aliendelea na elimu yake katika kozi ya uhandisi ngazi ya stashahada ambayo alisoma kwa muda wa miaka mitatu katika Chuo cha Ufundi Arusha.

Mmoja wa walimu wake, John Mbando, alitambua uwezo wake mapema na kumtia moyo katika fani hiyo kisha kumshawishi kuachana na uhandisi wa ujenzi na kubobea katika uhandisi wa mitambo.

Mbando alimshawishi kuwa uhandisi wa mitambo una manufaa mengi, ikiwa ni pamoja na kuwa na uhakika wa ajira, manufaa na kubuni vitu mbalimbali ambavyo vinatatua changamoto au matatizo yanayoikumba jamii.

Hali hiyo ilisababisha mapenzi ya Siah katika uhandisi wa mitambo kuongezeka na alidhamiria kuingia katika taaluma hiyo.

Baada ya kuhitimu vizuri stashahada yake, Siah alisoma kwa miaka mitatu katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ambako alihitimu Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Mitambo na kupata alama zenye wastani wa (GPA) 4.3 na kutunukiwa tuzo ya Mwanafunzi Bora wa Kike aliyehitimu mwaka wa kuhitimu 2019.

Mwalimu wa Siah, Mbando ndiye aliyefanikisha safari muhimu ya mwanadada huyo ambaye sasa ni mhandisi mbobevu.

Hakumfundisha tu ujuzi wa kiufundi wa uhandisi wa mitambo, bali pia alimjengea dhima nzima ya umuhimu wa kuzingatia maadili, mawasiliano na kufanya kazi kwa pamoja.

Alimhimiza kufuata ndoto zake na kamwe asikate tamaa, hata anapokabiliwa na changamoto. Uzoefu wa Siah ni ushuhuda wa nguvu ya ushauri na athari ambayo mwanamke au mtu yeyote anaweza kuwa nayo kwenye kazi na maisha ya kila siku.

Baada ya kumaliza masomo yake, Siah aliajiriwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa ajili ya mafunzo ya ufundi mitambo kama mhandisi wa mitambo.

Leo, anafanya kazi kama Mratibu 2 - katika idara ya inayoundwa na timu ya wahandisi. Anafurahi kuwa sehemu ya kampuni hiyo inayojitolea kuwajibika kwa kwa jamii kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo zaidi wafanyakazi wake bila kujali jinsia huku ikiendelea na shughuli za uchimbaji madini mkoani Geita.

Ndani ya GGML, Siah amepata fursa ya kufanya kazi katika miradi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kubuni na kutekeleza ufumbuzi wa nishati endelevu.



Siah Malle (kushoto), akitoa tathmini ya miradi ya kiuhandisi iliyobuniwa na wahandisi vijana wa kike katika maonesho na kongamano la 8 la Wanawake Wahandisi Tanzania (TAWECE) yaliyofanyika Zanzibar hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Akiwa jaji katika maonesho hayo ya TAWECE 2023 yaliyofanyika visiwani Zanziba, Siah alikabidhiwa jukumu hilo muhimu katika kukuza usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake vijana kutimiza ndoto zao katika fani ya uhandisi.

Alikagua miradi ya uhandisi iliyowasilishwa na wahandisi wachanga wa kike na kutoa maoni na mwongozo muhimu kwao ili kupiga hatua kumfikia na hata zaidi yake.

Siah alifurahishwa na mawazo ya kiubunifu yanayoibua suluhu kwa matatizo mbalimbali ya jamii. Alishuhudia mawazo muhimu ya kibunifu kama vile miradi ya uzalishaji nishati inayotokana na jua, pikipiki za kibunifu za matairi mawili zinazotumika katika kusafirisha abiria mijini na programu zingine za kurahisisha maisha kwa binadamu.

Miradi hii ilionesha uwezo wa uhandisi kushughulikia changamoto za ulimwengu halisi na kuboresha maisha ya watu.

Siah anasema anajivunia kuwa sehemu ya hafla hiyo iliyopinga dhana potofu za kijinsia na kuvunja vizuizi dhidi ya wanawake kuingia katika fani ya uhandisi.

Anaamini matukio kama vile TAWECE ni muhimu katika kuhamasisha wanawake na wasichana wengi zaidi kufuata taaluma ya uhandisi, kuondokana na dhana potofu za kijinsia kwamba baadhi ya fani zinatakiwa kuhusishwa na wanaume pekee.

Hizi ni pamoja na ujuzi wa kiufundi, ujuzi wa kutatua matatizo, ubunifu na uvumbuzi, ujuzi wa mawasiliano, mawazo bora na usimamizi thabiti wakati mnafanya kazi ya pamoja.

Siah pia anasisitiza umuhimu wa uadilifu, uwazi na maendeleo ya kitaaluma, pamoja na haja ya wahandisi kufahamu maendeleo ya sasa yanayoendena na mabadiliko ya teknolojia.

Mradi wa ndoto yake ni kubuni mfumo ambao utaibua utatuzi changamoto mbalimbali zinazoikwamisha sekya ya madini, mradi ambao pia mbali na kuongeza ufanisi katika sekta hiyo, pia utainufaisha GGML na sekta ya madini kwa ujumla.

Safari ya Siah kama mhandisi wa kike ni msukumo chanya kwa wanawake wote. Kwa msaada wa walimu wake, washauri na mwajiri, ameshinda changamoto na kutekeleza ndoto zake, akiwawezesha wengine waliotaka kuishia njiani.

Historia yake ni ushuhuda wa ushauri unaweza kuwa na nguvu ya kubadilisha maisha ya mtu pindi anapoamua kujitolea na kuongeza bidii katika maisha ya kia siku.

Ushauri alioupata Siah ni kama ukumbusho kwamba wanawake wanaweza kufaulu katika nyanja zinazotawaliwa na wanaume kama vile uhandisi kwenye sekta ya madini.

# Wabaini uchimbaji madini hifadhi ya msitu

**Na Rahma Suleiman, aliyekua** MUHEZA

MSITU wa Hifadhi Asilia ya Amani-Nilo ulioko wilayani Muheza, mkoani Tanga, unakabiliwa na changamoto za uharibifu wa mazingira ikiwamo uchimbaji haramu wa madini katika vyanzo vya maji ndani ya hifadhi hiyo.

Kaimu Mhifadhi wa msitu huo, Alphonce Nyululu, aliyasema hayo ofisini kwake alipozungumza na waandishi wa habari cha Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) waliotembelea hifadhi wa msitu huo ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili.

Mhifadhi huyo alisema kwenye vianzio vya maji ndani ya msitu huo kuna madini ya dhahabu ya alluvia.

Madini ya dhahabu ya alluvia ni utajiri mkubwa na ni aina ya dhahabu inayopatikana katika udongo ulioachwa na maji yanayotiririka. Dhahabu hiyo huoshwa toka kwenye mwamba na kuwekwa kwenye mchanga au udongo karibu na mito au mabonde.

Mhifadhi huyo alisema changamoto nyingine ni uvunaji haramu wa mbao katika msitu huo kwa kukata miti mikubwa kwa ajili ya mbao.

Alisema msitu huo pia unakabiliwa na changamoto ya moto ambapo wakati wa kiangazi wakulima huandaa mashamba yao kwa kutumia moto na moto huo huruka na kuingia katika eneo la hifadhi ya msitu huo.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hizo, wana kikosi cha doria, lakini kikosi pekee hakiwezi kudhibiti uhalifu huo bila kushirikiana na wananchi wa vijiji vinavyozunguka msitu huo.

"Wananchi ndiyo wadhibiti wa kwanza na ndio maana katika vijiji 20 vinavyozunguka hifadhi asilia ya ya msitu huu, kuna kamati za ulinzi na usalama na kamati ya mazingira na hujipangia suala la doria na kujua kinachoendelea," alisema Nyululu.

Alisema kuwa akinaswa mhalifu anayehujumu msitu huo, kuna sheria ndogo za vijiji ikiwamo kulipa faini, akishindwa kutekeleza adhabu, sheria za nchi huchukua mkondo wake.

Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, alisema waandishi wa habari wana nafasi kubwa ya kutoa habari kwa umma kuhusu umuhimu wa misitu pamoja na viumbe hai vinavyopatikana.

Alisema bila kuwapo misitu huo, kuna hatari taifa kupoteza viumbe hai walioko na vyanzo vya maji vitakauka.

# Nguvu Moja ilivyong'ara tuzo barani Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya maeneo yaliyoshindanishwa ni pamoja na sekta za ujenzi, uendeshaji milki za nyumba (Estate management), huduma kwa watalii, nishati, kilimo biashara, ulinzi, usalama, operesheni za uokoaji na nyingine.

"Katika nyanja ya ulinzi, usalama na operesheni za uokoaji kwa kampuni za ngazi ya kati (medium sized companies) kampuni ya Nguvu Moja Security Services (NgMSS) ya jijini Dar es Salaam, ilikuwa mshindi wa kwanza wa jumla. Ushindi huo unatokana na utafiti wa utoaji huduma za ulinzi, usalama na uokoaji kwa kampuni za kati barani Afrika," ilitangazwa wakati wa kutoa tuzo hiyo.

NgMSS ni kampuni gani, ina historia gani na kwa vigezo gani inaweza kutwaa ubingwa huu wa tuzo la ubora wa kampuni bora ya huduma za ulinzi, usalama na uokoaji barani Afrika au maarufu kama African Company of the Year Award (ACOYA) toleo la kwanza zilizofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni zikiwa zimesimamiwa na kampuni ya huduma za ushauri ya Eastern Star Consulting Group (Tanzania) Limited?

Taarifa zinaonyesha NgMSS, kampuni yenye makao makuu yake jijini Dar es Salaam ikiwa na cheti ya ubora wa huduma cha Shirika la Viwango la Kimataifa maarufu kama International Standards Organization (ISO9001:2015) certification.

Kwa asilimia 100 ni ya Kitanzania ikimilikiwa na kuendeshwa na Watanzania hasa wastaafu kutoka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), hasa kutoka kundi la wanejeshi wa vikosi maalum na makomandoo, wastaafu wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na maofisa na wapiganaji kutoka vyombo vingine vya ulinzi na usalama pia kutoka Jeshi la Akiba maarufu kama Sungusungu na Mgambo.

"Ni kwa mchanganyiko huu wa maofisa na wapiganaji kutoka katika majeshi tofauti hapa nchini ndio ambao umeiletea ushindi NgMSS, heshima ambayo pia inakwenda kwa taifa letu, vyombo vya ulinzi na usalama na Watanzania kwa jumla," alisema, Kamil Joseph Alphonse, Mratibu wa NgMSS ambaye ni Ofisa Mkuu wa kanda ya Dar es Salaam wa kampuni hiyo.

"Ni kutokana na kazi nzuri, nidhamu na weledi wa wana NgMSS ndiyo umewafanya watayarishaji wa tuzo hizi ambazo zimeshirikisha mataifa kadhaa ya Afrika na kusimamiwa na kampuni ya ushauri ya Eastern Star Consulting Group (Tanzania) Limited chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mtendaji, Degratius KILAWE, umewafanya kuona kuwa NgMSS ina sifa zote za kuwa mshindi wa jumla katika huduma za ulinzi, usalama na operesheni za uokoaji," alitamba Alphonse.



Mratibu wa Nguvu Moja Security Services, Camil Alphonse (katikati), akionyesha tuzo ya ACOYA ambayo kampuni yake ilishinda. Wengine ni Irine Henry (kushoto) na Eugenia Alex (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Rekodi zinaonyesha NgMSS kwa vipindi mbalimbali na kwa sasa ilitoa huduma za ulinzi kwa kampuni kubwa za migodi ya kuchimba madini kama Tanzanite One ya Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, pia kampuni za Barrick Gold Mine (North Mara) inayomilikiwa kwa ubia na Serikali ya Tanzania kupitia Twiga Minerals Corporation na Pangea Gold Mine (Buzwagi) ambayo pia ilikuwa ikimilikiwa kwa ubia na serikali kupitia Twiga Minerals Corporation.

Kampuni zingine ni Buckreef Gold Mine ya Geita ambayo ni mbia na kampuni ya TRX ya nchini Canada na ambayo pia inamilikiwa na Serikali ya Tanzania kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na kampuni ya kuchimba madini ya Kichina ya ZEM Tanzania iliyopo wilayani Butiama katika mkoa wa Mara.

"Tunaiona tuzo ya ACOYA kuwa ni motisha unaotuhamasisha kufanya vizuri zaidi katika kuwahudumia wateja wetu na pia tuwekeze zaidi kwa wafanyakazi wetu na kufanya uwekezaji zaidi katika vitendea kazi vya kutekeleza majukumu yetu ya ulinzi, usalama na operesheni za uokoaji," alidokeza Alphonse wakati wa mkutano na waandishi wa habari kutangaza mafanikio ya tuzo ya ACOYA.

Kuthibitisha kuwa NgMSS ilipata tuzo kwa kustahili, Alphonse alisema baadhi ya maeneo ambayo kampuni ya Eastern Star Consulting Group (Tanzania) Limited waliyatazama katika kuamua mshindi wa tuzo ni pamoja na uwekezaji wa kutosha katika vifaa na mitambo ya ulinzi, usalama na operesheni za uokoaji, motisha kwa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa vya kujikinga kwa wafanyakazi maarufu kama Personal Protection Equipment (PPE).

Rekodi zinaonyesha kutokana na NgMSS kuwa na ubora na kuzingatia viwango vya afya na usalama maeneo ya kazi, Wakala wa Usimamizi wa Afya na Usalama Kazini (OSHA) iliitunuku NgMSS tuzo na hati za ubora kwa miaka miwili mfululizo kwa mwaka 2022 na 2023 katika sherehe za wafanyakazi duniani zilizofanyika kitaifa Dodoma na Morogoro mtawalia ambapo Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Profesa Joyce Ndalichako alikabidhi tuzo hizo kwa uongozi wa NgMSS.

Akizungumza katika sherehe ya kukabidhi tuzo kwa washindi, Balozi wa Msumbiji nchini, Pedro Azevedo Davane, aliwataka washindi wa tuzo hizo watumie ushindi huo kuwa chachu ya kuvuka mipaka ya Tanzania na kwenda kufanya biashara katika nchi nyingine nje ya mipaka ya Tanzania.

"Miaka miwili iliyopita viongozi wa Afrika walikutana pale jijini Kigali, Rwanda na kupitisha makubaliano ya mkataba wa biashara huru barani Afrika maarufu kama African Continental Free Trade Area (AfCFTA). Nachukua nafasi hii kuwahimiza sasa ndiyo muda wa kutafsiri kwa vitendo mkataba wa soko huria wa AfCFTA kwani tuzo za ACOYA zinathibitisha huduma na bidhaa zenu zinafikia kiwango cha kimataifa, sasa ni vema muende kufanya biashara Msumbiji, Senegal, Morocco, Afrika Kusini, Misri na Nigeria," alisema Balozi Davane.

Balozi Davene, aliwapongeza kampuni ya Eastern Star Consulting Group Limited chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mtendaji, Deogratius Kilawe, kwa kuja na ubunifu wa kushindanisha ubora wa huduma za kampuni ya kiafrika na kuchagiza biashara baina ya kampuni za Kiafrika ndani ya bara la Afrika.

"Mmepata tuzo ya African Company of the Year Awards (ACOYA) hii maana yake huduma zenu na bidhaa zenu zinaweza kuuzwa katika bara lote la Afrika, sasa nendeni tena kwa nguvu sana kufanya biashara hadi katika nchi za Ghana, Tunisia, Togo, Senegal, Ethiopia, Namibia, Misri, Afrika Kusini na hata Gabon," alimaliza Balozi Davane.

Kiwale alisema kampuni ya Eastern Star Consulting Group (Tanzania) Limited ni kampuni ya Kiafrika yenye dhamira ya kuyapa kampuni ya Kiafrika nafasi ya kutambua ubora wa huduma na bidhaa zao na kuyapa jukwaa la kujitangaza ili yaweze kuingia katika ushindani wa kibiashara barani Afrika jambo ambalo litanufaisha kampuni hayo na nchi za Kiafrika kwa ujumla.

Katika tuzo hizo jumla ya kampuni 149 ziliibuka washindi katika mashindano ambayo yalishirikisha zaidi ya kampuni 4,000 kutoka katika nchi kadhaa barani Afrika kwa uchache zikiwamo, Kenya, Afrika Kusini, Misri, Ghana, Ethiopia na nyingine.

NgMSS imechukulia ushindi wa tuzo za ACOYA kama chachu ya kuzidisha juhudi katika kazi za ulinzi, usalama na uokoaji kwa wateja wake katika vipindi vijavyo.

Rekodi zinaonyesha moja ya waliochangia mafanikio ya NgMSS ni mgodi wa kuchimba dhahabu wa Buck reef uliopo mkoani Geita ambao unamilikiwa kwa pamoja na kampuni kubwa la uchimbaji madini la TRX la Canada.

Mgodi wa Buckreef ambao pia unamilikiwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Kampuni ya uchimbaji madini ya Buck reef ina sera mahsusi ya kutoa kandarasi za kazi mbali mbali kwa kampuni za Kitanzania ili kusaidia ujenzi wa uchumi wa Tanzania. Moja ya kampuni zilizonufaika na sera hiyo ya Buck reef ni NgMSS.

Katika mtandao wa www.nguvumoja ulinzi.co.tz mtu anaweza kupata taarifa zaidi za Nguvu Moja Security Services.

# Marekani, Japan, Korea kushirikiana kiusalama

**WASHINGTON, Marekani**

NCHI za Marekani, Japan na Korea Kusini zimekubaliana kuhusu mpango mpya wa usalama utakaowezesha mataifa hayo matatu kushauriana wakati wa tukio lolote la mgogoro wa kiusalama au tishio katika eneo la Pasifiki.

Kwa mujibu wa ofisa kutoka serikali ya Rais wa Marekani, Joe Biden, aliyezungumza kwa sharti la kutotajwa jina, mataifa hayo matatu yamekubaliana kuwa wamoja wakati wa tishio ama mgogoro.

Pia alisema mpango huo haukiuki haki ya kila taifa ya kujilinda chini ya sheria ya kimataifa wala haubadilishi makubaliano yaliyomo kwenye mkataba wa pande mbili kati ya mataifa mawili ya Marekani na Japan na Marekani na Korea Kusini.

Inaelezwa kuwa Marekani ina zaidi ya wanajeshi 80,000 katika mataifa hayo mawili. Na kwamba lengo la Rais Biden ni kwa mataifa hayo kuimarisha usalama na ushirikiano wa kiuchumi.

Aidha, ilibainishwa kuwa chini ya uongozi wa Kishida na Yoon, Japan na Korea Kusini zimeanza kukaribiana tena.

Wapinzani hao wa kihistoria waligawanywa na maoni tofauti kuhusu historia ya vita vya pili vya dunia na utawala wa kikoloni wa Japan katika rasi ya Korea kutoka mwaka 1910 hadi 1945.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa chini ya uongozi wa Kishida na Yoon, mataifa hayo mawili yameanza kukaribiana tena huku viongozi hao wakikabiliana na changamoto za pamoja za kiusalama kutoka kwa Korea Kaskazini na China.


Viongozi wote wawili wameghadhabishwa na kuongezeka kwa majaribio ya makombora ya Korea Kaskazini na mazoezi ya kijeshi ya China karibu na kisiwa cha Taiwan kinachojitawala ambacho kinadaiwa na China kama sehemu ya eneo lake.

Wakati wa mkutano huo wa kilele, viongozi hao watatu, pia wanatarajiwa kueleza kwa kina teknolojia ya mawasiliano ya dharura ya pande tatu wakati wa mzozo na kutoa taarifa kuhusu hatua ambazo nchi hizo zimechukuwa za kushirikishana taarifa za onyo la mapema kuhusu kurushwa kwa makombora kutoka Korea Kaskazini.

Matangazo mengine ni pamoja na mipango ya kupanua ushirikiano wa kijeshi kuhusu ulinzi wa makombora na kulifanya kongamano hilo kuwa hafla ya kila mwaka.

Mshauri wa usalama wa kitaifa wa Biden Jake Sullivan, alisema viongozi hao, pia watajitolea kwa mchakato wa mipango ya miaka mingi ya mazoezi ya pamoja ya kijeshi.

**DW**



Ujumbe wa ECOWAS baada ya kukutana na Rais wa Niger, Mohamed Bazoum, aliyepinduliwa madarakani juzi.
**PICHA: MTANDAO**

# Idadi waliojeruhiwa yafikia 144 Ukraine

**KYIV, Ukraine**

POLISI nchini Ukraine imesema idadi ya watu waliojeruhiwa kutokana na kombora la Russia lililopiga ukumbi wa michezo katika mji wa Chernihiv Ukraine wamefikia 144 kati yao watoto wakiwa ni 15.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na maofisa hao miongoni mwa waathiriwa walikuwa watu ambao walikuwa wakisherehekea sikukuu ya Wakristo wa Orthodox kanisani na kwamba uwanja mkuu na jengo la chuo kikuu pia viliharibiwa katika shambulio hilo.

Aidha, ilielezwa kuwa Umoja wa Mataifa (UN) ulilaani tukio hilo, huku Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky akiapa jibu thabiti la wanajeshi wa Ukraine kwa shambulio la kigaidi.

Ilielezwa kuwa Chernihiv iliyoko kilomita 50 kusini mwa mpaka wa Ukraine na Belarus, ilizingirwa na wanajeshi wa Russia katika miezi michache ya kwanza ya uvamizi kamili wa Rais Vladimir Putin Februari 2022.

Kaimu meya wa Chernihiv, Oleksandr Lomako, aliiambia BBC kwamba jumba la maonyesho la jiji lilipigwa moja kwa moja. Na kwamba lilikuwa likiandaa mkusanyiko wa watengenezaji ndege zisizo na rubani.

"Ninaelewa kuwa lengo lao lilikuwa tukio la kijeshi linalofanyika katika jengo la jumba la maigizo, lakini ni wazi kwamba Warussia waliokuwa wakirusha makombora hayo na wale waliokuwa wakiwapa amri katikati ya siku kwa mji wa kiraia waligundua kwamba waathiriwa watakuwa raia," alisema Lomako.

"Hakuna njia nyingine ya kutafsiri zaidi ya uhalifu wa kivita dhidi ya raia, lakini uhalifu mwingine wa kivita wa Russia," alisema.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ukraine, Ihor Klymenko, alisema kwamba wote waliokuwa ndani ya jumba hilo la maonesho walifanikiwa kufikia makazi kwa wakati.

Alisema kuwa wengi wa waathiriwa walikuwa kwenye magari yao au kuvuka barabara wakati wa shambulio la roketi na vile vile wakirejea kutoka kanisani.

**BBC**

# ECOWAS yakutana na Bazoum

**NIAMEY, Niger**

SIKU moja baada ya mkutano wa wakuu wa majeshi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS), ujumbe kutoka taasisi hiyo ya kikanda uliwasili Niamey nchini Niger na kufanikiwa kukutana na Rais Mohamed Bazoum aliyepinduliwa madarakani.

Inaelezwa kuwa ujumbe huo wa ECOWAS uliwasili mjini Niamey juzi, ulipokelewa kwenye uwanja wa ndege na Waziri Mkuu aliyeteuliwa na viongozi wa mapinduzi, Mahamane Zeine.

Wakiongozwa na rais wa zamani wa Nigeria, Abdulsalami Abubakar, wawakilishi wa jumuiya hiyo ya Afrika Magharibi walikutana na Rais Mohamed Bazoum, aliyepinduliwa Julai 26, mwaka huu.

Inaelezwa kuwa mkutano huo ulifanyika mbele ya Waziri Mkuu aliyeteuliwa na viongozi wa mapinduzi na mjumbe mwingine wa utawala huo wa kijeshi.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa hakuna habari iliyofichuliwa kuhusu mazungumzo yao na kwamba wajumbe wa ECOWAS walikuwa wameenda kuona mazingira ambayo rais aliyepinduliwa anazuiliwa.

Pia ujumbe huo awali ulikutana na wajumbe wa serikali ya kijeshi, akiwamo Jenerali Tiani. Na kwamba walikuwa na ujumbe kurejeshwa kwa utawala wa kikatiba nchini Niger.

Kulingana na mmoja wa wajumbe wa ECOWAS, kwa ombi la utawala wa kijeshi, mkutano mwingine na rais wa zamani wa Niger, Mahamat Issoufou, ulijumuishwa katika mpango huo.

Ilielezwa kuwa ujumbe huo ulijumuisha mwenyekiti wa Tume ya ECOWAS. Na kwamba ni ujumbe ambao ulifanya ziara yake ya kwanza kwenda Niamey baada ya mapinduzi.

Vile vile, ilielezwa kuwa ulipokelewa vibaya na haukuweza kuondoka kwenye uwanja wa ndege.

Kwa mujibu wa RFI, Rais wa Togo, Faure Gnassingbé, alitekeleza jukumu la busara ili Niamey, wakati huu, ifungue milango yake kwa upana kwa wajumbe kutoka Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi.

**RFI**

**Pia ujumbe huo awali ulikutana na wajumbe wa serikali ya kijeshi, akiwamo Jenerali Tiani. Na kwamba walikuwa na ujumbe kurejeshwa kwa utawala wa kikatiba nchini Niger.**

HABARI MICHEZO

# KMKM YAANIKA SABABU KICHAPO CAF IKIITAFUTIA DAWA ST GEORGE

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya KMKM ya Zanzibar, umesema kukosekana kwa wachezaji wao wanne wa kigeni kutokana na kutokamilika kwa vibali vyao vya Kimataifa (ITC), ndicho kilichoigharimu timu yao na kupoteza mchezo wao wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya St. George ya Ethiopia, lakini tatizo hilo kwa sasa wamelitatua jambo linalowapa matumaini kuelekea mechi ya marudiano ugenini.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanjwa wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, KMKM ilikubali kipigo cha mabao 2-1, hivyo inapaswa kwenda kupindua meza katika mechi ya marudiano Ethiopia ili kusonga mbele.

Akizungumza na Nipashe jana, Naibu Katibu Mkuu wa KMKM, Suleiman Rajabu, alisema changamoto hiyo ilichangia kuvuruga malengo ya benchi la ufundi, hivyo kulazimika kutumia wachezaji wengine.

Alisema taratibu za kukamilisha vibali vya wachezaji hao zinaendelea vema na kuweka wazi mpaka kufikia kucheza mchezo wa marudiano nchini Ethiopia Agosti 27, mwaka huu vitakuwa tayari.

"Kukosekana kwa wachezaji wetu hao kumechangia kwa kiasi kikubwa tuanze vibaya mashindano hayo, naamini mpaka ifike Agosti 27 katika mchezo wa marudiano kila kitu kitakaa sawa," alisema Rajabu.

Alisema kikosi chao kitaendelea kubaki jijini Dar es Salaam kwa lengo la kutafuta mchezo mmoja wa kirafiki ili kuwaweka sawa wachezaji kabla ya kuanza safari kuelekea nchini Ethiopia Ijumaa wiki hii.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa KMKM, Masoud Djuma, alisema bado ana kazi kubwa ya kufanya kwenye safu yake ya ushambuliaji kuelekea mechi ya marudiano wiki hii.

Akizungumza na Nipashe jana, Masoud alitaja mambo mawili ambayo yaliyowaangusha kwenye mechi ya kwanza kwamba ni kushindwa kutumia nafasi nyingi walizozitengeneza pamoja na wachezaji wake kukosa uzoefu kwenye michuano ya kimataifa. Alisema suala la ushambuliaji analifanyia kazi ili kuhakikisha wachezaji alionao wanaweza kumpa kitu katika mchezo wa marudiano.

'Tunawakosa washambuliaji wetu wanne hawana vibali (ITC), tumelazimika kubadilisha baadhi ya wachezaji kuwa wafungaji, naifanyia kazi safu hiyo kwa kuwaongezea mbinu ili kupata matokeo mazuri mechi yetu ya marudiano.

"Naamini haitakuwa mechi rahisi, ila ninaimani kubwa na wachezaji wangu kubadilisha matokeo dhidi ya St George, hii ni kutokana na mechi ya juzi kipindi cha pili kucheza vizuri na kutawala mchezo," alisema Masoud.

VYOMBO...



Wanafunzi wa Shule ya Kibaha Adventist Primary School (KAPS), wakionyesha uwezo wa kupiga vyombo vya muziki walipokuwa wakiimba katika Kanisa la Waadventista Wasabato Mbezi Luis Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Tabora United sasa kamili Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa timu ya Tabora United (Kitayosce FC), umesema tayari wameshughulikia suala la wachezaji wao wa kimataifa na sasa watakuwapo kwenye mchezo wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Fountain Gate FC utakaopigwa Agosti 31, mwaka huu.

Katika mechi ya kwanza ya ligi hiyo, Tabora United walishindwa kutumia wachezaji wao wakigeni akiwamo Papy Tshishimbi aliyewahi kuichezea Yanga, nyota wengine ni Andy Bikoko kutoka DR Congo, Toauya Jean (Burundi) na Mkongomani Lumiere Banza aliyekuwa akiichezea TP Mazembe.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa timu hiyo, Rashid Hassan, alisema baada ya kutokea sintofahamu kwa kuwakosa wachezaji wao wa kigeni katika mchezo dhidi ya Azam FC kutokana na majina yao kutokuwapo kwenye mfumo rasmi wa usajili, lakini kwa sasa tayari wameshafanyia kazi tatizo hilo na mechi dhidi ya Singida Fountain Gate FC watakuwa miongoni mwa watakaounda kikosi cha timu hiyo.

Alisema kulikuwa na changmoto ya kiuongozi na ameshafanyia kazi na tayari wachezaji na timu hiyo wameweka kambi Morogoro kwa ajili ya maandalizi ya mechi yao dhidi ya Singida Fountain Gate utakaopigwa Agosti 31, mwaka huu.

"Kila kitu kimekwenda vizuri wachezaji wetu wapya tuliowasajili tumeshawaingiza kwenye mfumo na tunajipanga kwa mechi ijayo ya ligi kuhakikisha tunafanya vizuri na kupata matokeo mazuri baada ya kupoteza mechi ya kwanza dhidi ya Azam FC," alisema Meneja huyo.

Naye Kocha Mkuu wa kikosi cha timu hiyo, Goran Kopunovic, alisema kabla ya kwenda kuweka kambi Morogoro alifanya kikao na viongozi wake na kumhakikishia hakutakuwa na changamoto yoyote ya kukosa wachezaji katika mechi ijayo.

Pia alizungumzia suala lake la kimkataba na kuahidiwa kufanyia kazi kwa kukamilishiwa kile ambacho walikubaliana katika mkataba wao walioingia.

"Nimezungumza na viongozi wangu kuhusu makubaliano yetu, lakini mustakabali wa timu kwa wachezaji ambao tumewasajili kuhakikisha kila kitu kinaenda vizuri niweze kuwatumia kwenye mechi yetu ijayo dhidi ya Singida Fountain Gate FC, limefanyiwa kazi na sasa tupo Morogoro kwa ajili ya maandalizi," alisema Kocha Goran.

# Watoto 9 wavunja rekodi kuogelea

**Na Shufaa Lyimo**

WATOTO tisa wenye umri kuanzia miaka sita na kuendelea, wamevunja rekodi kwenye mashindano ya Kuogelea Kupunguza Muda (HPT), yaliyofanyika katika Bwawa la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST), Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa timu ya Kuongelea, Michael Livingstone, alisema watoto wengi wameonesha viwango kwenye mashindano hayo ambayo yalishirikisha watoto 98 kutoka klabu mbalimbali nchini.

"Watoto wengi wameonyesha uwezo mzuri katika mashindano hayo ambayo yalikuwa na ushindani mkubwa," alisema Livingstone huku akiwataja watoto hao kuwa ni Zainab Mosajee rekodi moja, Cressa Dillip rekodi mbili, Missokia Max rekodi ya tatu, Julius Missokia rekodi mbili pamoja na Saliboko Collins mwenye rekodi moja.

Kocha huyo alisema wachezaji hao ndio ambao watakwenda kushiriki mashindàno ya kimataifa, nchini Mauritius.

Kwa upande wa Meneja wa mashindano hayo, Francisca Binamungu, alisema lengo ni kukuza vipaji vya watoto ili kuwafikisha mbali kupitia mchezo huo.

Alisema mwaka huu mashindano hayo yameboreshwa tofauti na miaka iliyopita, kwa kutoa zawadi kwa washindi pamoja na fedha kwa wale waliovunja rekodi ili kuwapa morali ya kufanya vizuri zaidi.

"Tumekuwa tukifanya michezo mbalimbali hapa nchini lakini tumeamua tuanze na mchezo huu wa kuogelea vile vile tunalenga zaidi watoto kupunguza muda, wengi wamejitahidi na wameweza kuvunja rekodi," alisema Binamungu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CANCELO SAFI BARCA**
KUNA makubaliano kimsingi kwa mlinzi wa kulia wa Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 29, kujiunga na Barcelona kutoka Manchester City kwa mkopo wa awali wa msimu mzima. **(SPORT)**

**BALOGUN ATAKIWA CHELSEA**
CHELSEA imefanya mawasiliano na washauri wa mshambuliaji wa Marekani aliyekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 50, Folarin Balogun mwenye umri wa miaka 22. (TalkSport)

**TAVARES ANATAFUTA KWINGINE**
MLINZI wa kushoto wa Arsenal, Nuno Tavares mwenye umri wa miaka 23, anatafuta chaguzi nyingine baada ya pendekezo la kuhamia Nottingham Forest kuwa gumu. **(Fabrizio Romano)**

**ARSENAL YAMZUIA PARTEY**
ARSENAL haina nia ya kumuuza kiungo wa kati wa Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 30, huku kukiwa na nia kutoka Saudi Pro League pamoja na Juventus na Fenerbahce. (Express)

**MUANI ANUKIA PSG**
KLABU ya Paris St-Germain wamekubaliana maslahi binafsi na mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, Randal Kolo Muani mwenye umri wa miaka 24. (Foot **Mercato)**

**KUDUS NA WEST HAM**
KLABU ya West Ham United imetoa ofa ya kumnunua kiungo wa kati wa Ghana, Mohammed Kudus mwenye umri wa miaka 23, iliyokataliwa na Ajax. **(The Athletic)**

**STEGEN KUJIFUNGA BARCA**
GOLIKIPA wa Ujerumani, Marc-Andre ter Stegen mwenye umri wa miaka 31, anakaribia kusaini mkataba mpya na Barcelona ambao utamweka katika klabu hiyo hadi 2028. **(ESPN)**

**TIERNEY KURUDI CELTIC**
KLABU ya Celtic sasa ipo katika nafasi nzuri zaidi ya kumnunua tena mlinzi wa kushoto wa Arsenal, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 26, baada ya Newcastle United kuachana na nia yao ya kumnunua mlinzi huyo wa Scotland. **(Football Insider)**

**BISSAKA HATAONDOKA UTD**
AARON Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 25, hataondoka Manchester United msimu huu wa majira ya joto kwani anataka kupigania nafasi ya beki wa kulia kuwa chaguo la kwanza pale Old Trafford. **(Mail)**

**DE BEEK, WILLIAMS KUSEPA**
KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 26 na mlinzi wa kushoto wa England, Brandon Williams (22), wote wanaweza kuondoka Manchester United kwa sababu hawafikiriwi kwenye kikosi cha kwanza. **(Manchester Evening news)**

**PAVARD KUBAKISHWA INTER**
INTER Milan wanashinikiza kumsajili beki wa kulia wa Ufaransa, Benjamin Pavard kutoka Bayern Munich - lakini Thomas Tuchel anataka kumbakisha nchini Ujerumani beki huyo mwenye umri wa miaka 27. **(Sky Sports)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BECKHAM AKUNWA MESSI AKIWAPA TAJI LA KWANZA

Usiku wa leo (juzi) ulikuwa wa kipekee sana, nadhani, si kwa klabu yetu tu, lakini kwa mashabiki wetu, wachezaji na...

**NASHVILLE, Marekani**

MMILIKI mwenza wa Inter Miami CF, David Beckham, alitaja ushindi wa penalti wa timu yake dhidi ya Nashville SC katika fainali ya Kombe la Ligi ni "usiku wa kipekee sana" na akawasifu wamiliki wenzake, Jorge na Jose Mas kama "washirika kamili."

Miami ilianza kwa bao la Lionel Messi na Fafa Picault akasawazisha dakika ya 57 na kuufanya mchezo huo kwenda kwenye mikwaju ya penalti ambapo Inter Miami ilishinda 10-9, hivyo kutwaa taji lao la kwanza tangu ilipoanzishwa mwaka 2020.

"Usiku wa leo (juzi) ulikuwa usiku wa kipekee sana, nadhani, si kwa klabu yetu tu, lakini kwa mashabiki wetu, wachezaji, familia zetu na wafanyakazi wetu wote ambao wamehusika katika safari hii nasi," alisema Beckham.

"Lakini haikuwa rahisi. Usiku wa leo (juzi) ulikuwa mchezo mgumu sana. Nashville walifanya pambano la ajabu. Ilikuwa karibu sana mwishoni na pongezi kwao kama klabu, kama washirika na kama wachezaji, kwa sababu ilikuwa ngumu sana. Mchezo mgumu. Lakini ulikuwa ni usiku wetu tu usiku wa leo (juzi)."

Beckham alikumbuka ugumu wake katika mikwaju ya penalti, ikiwa ni pamoja na kukosa katika raundi ya mtoano dhidi ya Ureno kwenye euro 2004.

"Mimi si shabiki mkubwa wa penalti," alitania. Kisha akaongeza, "Si rahisi kamwe kutazama michezo hii ikiisha hivi. Na kwa timu ambazo haziishii kushinda, ni wakati mgumu. Lakini kila penalti ya Miami ilikuwa ya ajabu."

Beckham angeweza kuthamini ushindi huo zaidi ya mtu mwingine yeyote. Alianza harakati zake za kuweka timu ya upanuzi ya MLS huko Miami mnamo 2014, lakini akakumbana na vikwazo vingi katika kutafuta wawekezaji zaidi na pia njia ya mkataba wa uwanja.

Lakini bahati yake ilianza kubadilika mnamo 2017 alipokuja Jorge na Jose Mas kama wamiliki wenza.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
CRYSTAL PALACE
VERSUS
ARSENAL
1 | 5.10
X | 3.83
2 | 1.69

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG AONESHWA TOBO UNITED

**LONDON, England**

ERIK ten Hag amesema ni "dhahiri" kwa nini Manchester United ilisajili mshambuliaji msimu huu baada ya timu yake kuhangaika mbele ya lango kwenye kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Tottenham Jumamosi.

United walikuwa wazi juu ya hitaji lao la kuongeza mshambuliaji katika dirisha la uhamisho, huku ESPN ikiripoti hapo awali idara ya usajili ya klabu ilikuwa na hifadhi data ya washambuliaji karibu 1,800 mwanzoni mwa utafutaji wao.

Licha ya Harry Kane kuondoka Spurs msimu huu wa majira ya joto - akijiunga na Bayern Munich - United iliamua kumsajili Rasmus Højlund mwenye umri wa miaka 20, katika mkataba uliojumuisha ada ya pauni milioni 64, pamoja na pauni nyingine milioni nane katika nyongeza.

Baada ya kuona timu yake ikishindwa kufunga mabao ambayo ni pamoja na kusajili mashuti matatu pekee kati ya 14 yaliyolenga lango kipindi cha kwanza, Ten Hag alisema anaamini kikosi chake kina mabao, lakini alikiri kuwasili kwa Højlund, ambaye bado hajacheza mechi yake ya kwanza kutokana na kuumia, ni suala la muda.



"Tunaamini wachezaji hawa, mwaka jana pia, wanaweza kufunga mabao. Ni wazi pia kwa nini tulisajili mshambuliaji," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari.

"Kama yote yataenda vizuri, Marital yuko njiani kurudi, Højlund pia anakuja, kwa hivyo tutakuwa na wachezaji wengi wa kufunga mabao. Wachezaji uwanjani wanaweza pia kufunga mabao."

United waliibuka na ushindi mwembamba wa bao 1-0 dhidi ya Wolves Jumatatu iliyopita, huku matokeo ya Jumamosi yakiongeza mwanzo wao wa polepole wa msimu wa 2023-24 wa Ligi Kuu England.

Wakati huo huo, Spurs walicheza nyumbani kwa mara ya kwanza tangu wampoteze Kane, lakini walionesha onyesho la kuvutia kipindi cha pili ambalo lilimshuhudia kocha mpya Ange Postecoglou akipata ushindi wake wa kwanza akiwa kocha.

# Guardiola, shabiki chaumana

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema alimwomba shabiki wa Manchester City kuchukua nafasi yake kwenye benchi wakati wa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Newcastle United baada ya kukosolewa kwa kutofanya mabadiliko yoyote.

Guardiola alitoa ishara kwa shabiki karibu na benchi la City kuchukua nafasi yake kama kocha baada ya majibizano ya maneno.

Alifichua baadaye kuwa ni kwa sababu ya uamuzi wake wa kutofanya mabadiliko yoyote, ikiwa ni mara ya kwanza ameshindwa kufanya mabadiliko katika mchezo wa Ligi Kuu tangu Mei 2022.

"Alinitaka nifanye mabadiliko, mchezaji mmoja atoke na mwingine aingie, nikamuuliza yupi, sikujua," alisema Guardiola.

"Nilisema 'njoo hapa uifanye.' Niliona kwamba timu wakati huo ilikuwa bado



hai na wakati mwingine kuingia, mdundo ni mgumu.

"Niliona timu bado ipo na inapigania kila mpira. Wasimamizi, tunayo chaguo kufanya mabadiliko, lakini wasimamizi wanaamua au la."

Guardiola alisema kabla ya mchezo dhidi ya Newcastle alikuwa na wasiwasi baada ya kuwapoteza wachezaji kadhaa muhimu akiwamo Kevin De Bruyne kutokana na majeraha.

Hata hivyo, Julian Álvarez alifunga katika kipindi cha kwanza na kupata ushindi wa bao 1-0 na kuhakikisha City inadumisha mwanzo wao mzuri wa msimu kwa kushinda kwa mara ya pili mfululizo.

"Huu ni mchezo wa pili wa msimu huu, lakini ni uthibitisho wa sababu iliyotufanya tushinde sana," alisema Guardiola.

"Mawazo ya kundi hili la wachezaji hunishangaza kila wakati. Dhidi ya timu hiyo na hali tunayofikia, tukiwa na majeraha mengi na hakuna kupumzika, walicheza vizuri sana. Jinsi wanavyolinda na jinsi wanavyokimbia na kujitolea kwa kila mtu ilikuwa ya kushangaza kabisa."

Y | CHEZA USHINDE KASINO

# MAXIME ASHANGAA IHEFU KUTOWAPIGA MABAO MENGI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, ameishangaa Ihefu FC kwa kutofunga mabao mengi katika mechi ya juzi kutokana na makosa lukuki waliyoyafanya.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Highland, Mbarali mkoani Mbeya, Maxime alisema wamepoteza mechi hiyo kwa bao 1-0 kwa sababu moja tu kwamba hawakucheza vizuri na wamefanya makosa mengi.

Alisema kwa makosa waliyoyafanya walitakiwa wafungwe mabao mengi sana, lakini wapinzani wao, Ihefu wameshindwa kutumia udhaifu wao.

"Niwape pole wachezaji wangu, niwapongeze Ihefu kwa ushindi, lakini nashangaa kwa kutotufunga mabao mengi, hatukucheza mchezo mzuri, tulikuwa na mapungufu mengi sana, sitakiwa kusema maneno mengi, lakini Ihefu FC wamefaidika na makosa yetu," alisema Maxime.

Zipo taarifa kuwa Kagera Sugar walitua Mbarali usiku wakitokea Kigoma kwa basi, siku moja kabla ya kuamkia mechi hiyo, hivyo wachezaji wa timu hiyo walionekana wachovu.

Kocha Mkuu wa Ihefu, Zuberi Katwila, alisema kuwa Kagera Sugar hawakucheza vibaya na waliutawala mpira kipindi chote cha kwanza, ndiyo maana akalazimika kubadilisha mfumo baada ya mapumziko.

"Wenzetu walionekana kuja kwa kushambulia kwenye mechi ya leo na si kuzuia, ikabidi kipindi cha pili tukabadilisha 'plani' iliyozaa bao, kusema kweli ilikuwa mechi nzuri na nguku, Kagera Sugar siyo timu ya mchezo, kuifunga si jambo rahisi," alisema Katwila.

Ni mechi ya kwanza kwa Ihefu kushinda msimu huu baada ya kupoteza nyumbani bao 1-0 Jumanne iliyopita dhidi ya Geita Gold hivyo kuwa na pointi tatu mpaka sasa, huku Kagera Sugar ikipoteza mechi ya pili mfululizo baada ya Jumatano iliyopita kutwangwa mabao 2-0 dhidi ya Mashujaa FC na kutovuna pointi yoyote mpaka sasa.



Mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke, akijiandaa kuachia shuti langoni mwa Dodoma Jiji FC katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana na wenyeji hao kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba yaua na 'pira biriani' juu

INATOKA UK. 24

mguu wa kushoto bao lake la pili mfululizo kwenye Ligi Kuu.

Kipindi cha pili Simba iliwaingiza Miquissone, Sadio Kanoute, Kibu Denis, Israel Mwenda ambao waliibadilisha timu kwa kiasi kikubwa, huku Dodoma Jiji nao wakiwa wametoka langoni kwao kusaka bao la kusawazisha.

Haikushangaza Raizin Hafidh kukaribia kusawazisha dakika ya 49 kwa shuti kali lililopanguliwa na kipa Ally Salum, lakini Emmanuel Martin akifanya hivyo dakika ya 53.

Dodoma Jiji ikiwa na wachezaji wake mahiri kina Salmin Hoza, Gustavo Simon, David Kibuta, Mtenje Albano ilijitahidi kwa kila hali, lakini ukuta wa Simba, ukiongozwa na Che Fondon Malone akisaidiwa na Kennedy Juma, ulikaa imara.

Kazi nzuri iliyofanywa na Kapombe ya kukokota mpira winga ya kulia na kuuingiza ndani na kumkuta Phiri akiwa kwenye eneo zuri ambalo aliutuliza kisha akatisha kama anapiga, akausogeza pembeni kidogo na kuwahadaa mabeki pamoja na kipa, kabla ya kupiga shuti kwa mguu wa kulia akiwa ndani kidogo ya boksi, mpira ukajaa wavuni.

Licha ya kukosa mabao mengi, Simba jana iliwakumbusha mashabiki wake mpira wa pasi nyingi, kasi na mbwembwe 'pira biriani' ambalo liliwafanya kupagawa kwa furaha.

Ni matokeo yaliyowaweka Wekundu wa Msimbazi hao kileleni mwa msimamo wakiwa na pointi sita, mabao sita, ikiwa imeruhusu mawili.

Rekodi pia inaonesha wafungaji wote wa mabao hayo ni wageni, hivyo hakuna mzawa yeyote aliyefunga bao mpaka sasa.

# Yanga yaanza mauaji

INATOKA UK. 24

hiyo walionekana wako imara, lakini katikati ya uwanja upande wa viungo na washambuliaji wao ni maeneo ambayo walikosa kabisa mbinu za kuisumbua ngome ya Yanga.

Yanga ilifanya mabadiliko kipindi cha pili kwa nyakati tofauti, iliwaingiza Pacome Zouzoua, Hafiz Konkoni, Farid Mussa na Salum Aboubakar, lakini ndicho kipindi ambacho wapinzani wao walionekana kuchangamka.

ASAS ilipiga mashuti mawili tu kwa Yanga na ilikuwa dakika ya mwisho kabla ya mechi kumalizika kupitia kwa Ahmed Ally na Hemed Juma Traole ambayo yalikuwa ya hatari.

Timu hizo zitarudiana tena Agosti 26, mwaka huu kwenye uwanja huo huo, ambapo Yanga inahitaji sare, ushindi au kutofungwa zaidi ya bao moja ili kutinga raundi ya kwanza ambayo itaiwezesha kucheza na mshindi kati ya Otoho d'Oyo ya Congo Brazaville na El Merrikh ya Sudan ambapo mpaka tunakwenda mitamboni zilikuwa sare ya bao 1-1, mechi ikichezwa Brazaville.

Wakati Yanga ikiibuka na ushindi huo, Azam FC imepata kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Bahir Dar Kenema ya Ethiopia mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika ikipigwa katika Uwanja wa Abebe Bikila nchini humo, Idris Mbombo ndiye aliyeipatia Azam bao la kufutia machozi.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 21/08/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1325 | Seongnam Ilhwa vs Bucheon | 2.27 | 3.12 | 2.87 |
| 13:30 | 3294 | Gyeongnam vs Cheonan City FC | 1.51 | 3.90 | 5.26 |
| 14:30 | 2806 | Chonburi vs Khon Kaen United FC | 1.50 | 3.93 | 5.25 |
| 16:00 | 3448 | Mashujaa FC vs Geita Gold FC | 2.40 | 3.00 | 2.90 |
| 17:00 | 3181 | FC Andijon vs FC Olimpik | 2.44 | 2.83 | 2.88 |
| 17:00 | 5750 | KamAZ vs Arsenal Tula | 2.27 | 3.18 | 2.82 |
| 18:00 | 1996 | FC Struga Trim Lum vs Akademija Pandev | 1.50 | 3.82 | 5.90 |
| 18:00 | 2940 | FK Kauno Zalgiris B vs FK Vilnus Bfa | 3.12 | 3.47 | 1.99 |
| 18:00 | 3218 | FC KTP vs Haka | 2.52 | 3.23 | 2.47 |
| 18:00 | 5419 | Vmfd Zalgiris vs 3-FK Silas | 2.14 | 3.44 | 2.83 |
| 18:00 | 5476 | FK Sloga Simin Han vs FC Sarajevo | 1.88 | 3.51 | 3.51 |
| 18:30 | 1272 | FC Honka/Akatemia vs Atlantis FC | 2.75 | 3.82 | 2.11 |
| 18:30 | 2232 | NK Jarun Zagreb vs Orijent Rijeka | 2.11 | 3.28 | 3.03 |
| 18:30 | 2400 | Sepsi Osk vs Hermanstadt | 1.98 | 3.23 | 3.64 |
| 19:00 | 3258 | Znicz Pruszkow vs GKS Katowice | 2.67 | 3.17 | 2.38 |
| 19:24 | 2202 | Torpedo Moscow vs Neftekhimik | 1.69 | 3.39 | 4.46 |
| 19:30 | 1227 | Torino vs Cagliari | 1.70 | 3.73 | 5.18 |
| 19:30 | 1293 | Le Mans vs Dijon | 2.21 | 3.35 | 2.99 |
| 20:00 | 1433 | Villarreal B vs CD Eldense | 2.03 | 3.51 | 3.21 |
| 20:00 | 2669 | Viborg FF vs Vejle BK | 1.70 | 3.66 | 4.72 |
| 20:00 | 3283 | Cracovia vs GKS Piast Gliwice | 2.78 | 3.03 | 2.38 |
| 20:00 | 3295 | Kristianstads FF vs IFK Malmo | 1.76 | 3.76 | 3.76 |
| 20:00 | 4415 | Alaves vs Sevilla FC | 3.30 | 3.04 | 2.39 |
| 20:00 | 4544 | Omonia Nicosia vs Nea Salamis | 1.69 | 3.63 | 4.67 |
| 20:00 | 5273 | Doxa Katokopia vs AEL Limassol | 2.36 | 3.27 | 2.85 |
| 20:10 | 1234 | Norrkoping vs AIK Football | 2.25 | 3.22 | 2.82 |
| 20:45 | 4545 | SCU Torreense vs Nacional Madeira | 2.24 | 3.27 | 2.92 |
| 21:00 | 1018 | Jong Ajax vs De Graafschap | 2.41 | 3.38 | 2.61 |
| 21:00 | 1721 | Sport Boys Association vs Atletico Grau | 2.02 | 3.23 | 3.28 |
| 21:00 | 2342 | Eyupspor vs Kocaelispor | 1.75 | 3.53 | 3.94 |
| 21:00 | 2477 | Aegir vs Grotta | 3.53 | 3.89 | 1.76 |
| 21:00 | 3065 | Fjolnir vs UMF Grindavik | 1.75 | 3.73 | 3.68 |
| 21:00 | 3404 | Samsunspor vs Fenerbahce | 4.61 | 3.93 | 1.63 |
| 21:00 | 3547 | Defensores Unidos vs Temperley | 3.10 | 2.85 | 2.34 |
| 21:00 | 3740 | Jong Utrecht vs Groningen | 4.41 | 3.75 | 1.66 |
| 21:00 | 5575 | Ankaragucu vs Adana Demirspor | 2.49 | 3.72 | 2.42 |
| 21:15 | 4637 | Debreceni VSC vs Kisvarda FC | 2.79 | 3.25 | 2.30 |
| 21:30 | 1327 | El Porvenir vs CA Lugano | 2.22 | 3.11 | 3.05 |
| 21:30 | 3960 | Universitatea Cluj vs CFR Cluj | 3.80 | 3.29 | 1.91 |
| 21:45 | 1566 | Bologna vs AC Milan | 3.87 | 3.46 | 1.99 |
| 21:45 | 5287 | AC Ajaccio vs Bordeaux | 2.19 | 3.02 | 3.32 |
| 22:00 | 1004 | Crystal Palace vs Arsenal | 5.10 | 3.83 | 1.69 |
| 22:15 | 1761 | Famalicao vs Moreirense | 2.09 | 3.09 | 3.54 |
| 22:15 | 3344 | Stjarnan vs KR Reykjavik | 2.02 | 3.61 | 3.05 |
| 22:30 | 2963 | Granada vs Rayo Vallecano | 2.50 | 3.13 | 3.03 |
| 22:30 | 3609 | Huesca vs Tenerife | 2.63 | 2.92 | 2.72 |
| 22:30 | 3670 | San Martin SJ vs San Martin Tucuman | 2.32 | 2.94 | 3.04 |
| 22:45 | 3944 | Leixoes vs Santa Clara | 2.66 | 3.28 | 2.42 |
| 23:15 | 2775 | UTC Cajamarca vs Escuela Municipal Deportivo Binacional | 1.78 | 3.47 | 3.83 |
| 23:30 | 1557 | Tigres FC (COL) vs Orsomarso | 1.66 | 3.31 | 5.10 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

%%%%%%

# Michezo

Jumatatu Agosti 21, 2023


Nipashe





Beckham akunwa Messi akiwapa taji la kwanza UKURASA 21


MILIKI...



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Pacome Zouzoua, akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa ASAS ya Djibouti, kwenye mechi ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda mabao 2-0. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA YAANZA MAUAJI CAF, AZAM YADUNDWA

## ●●●Aziz Ki, Musonda wawapa raha Wananchi, sasa wasubiri kumaliza kazi...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya wachezaji wa kimataifa, Mburkina Faso Stephane Aziz Ki na Mzambia Kennedy Musonda, yameifanya Yanga kuondoka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya ASAS Ali Sabieh ya Djibouti katika mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika.

Mechi hiyo iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, kikanuni ilihesabika kuwa Yanga inacheza ugenini baada ya Wadjibouti hao kuamua mchezo wake wa nyumbani kuchezea hapa nchini.

Baada ya kukosa mabao ya wazi dakika ya tisa na sekunde chache baadaye, hatimaye Aziz Ki alipachika bao dakika ya 21 kwa mguu wa kushoto akiwa ndani ya eneo la hatari, alipopokea krosi kutoka kwa winga wa kushoto, Joyce Lomalisa, ambaye alipanda kusaidia mashambulizi.

Mpira ulianza katikati ya uwanja kwa Khalid Aucho ambaye aliupelekea pembeni kwa Maxi Nzengeli, aliupokea na kugeuka, akavuta hatua kadhaa kabla ya kumpenyezea mtoa pasi, Lomalisa.

Kabla ya hapo, tayari Musonda alikuwa amekosa bao la wazi dakika ya 15 akiunganisha kwa kichwa mpira wa krosi, lakini ukatoka nje, Clement Mzize naye akikosa dakika moja baadaye.

Sifa za pekee kwenye mechi ya jana zilimwendea kipa raia wa Burundi, Innocent Mbonihankuye, ambaye aliokoa hatari na michomo mingi, vinginevyo Yanga ingeweza kuondoka na ushindi mnono kwenye mechi hiyo.

Mudathir Yahya ni mmoja kati ya wachezaji walioonja chungu ya kipa huyo, kwani alikosa mabao matatu ya wazi ambayo kipa huyo aliokoa.

Bao la pili lilifungwa dakika ya 52 na Musonda aliyepokea pasi ndefu na kumzidi mbio mmoja wa mabeki wa ASAS kwenye wingi ya kushoto, nia yake ikiwa kupiga krosi, lakini shuti lilikatika na kwenda kugonga kwenye maungio ya mwamba wa juu na wa chini upande wa kushoto kwa kipa Mbonihankuye na kujaa wavuni.

Baada ya hapo Yanga iliendelea kutawala mchezo, ikionekana kusaka mabao mengi, lakini mabeki wa ASAS na kipa wao walikaa imara.

Kuanzia kipa mpaka mabeki wa timu


INAENDELEA UK. 20


## Simba yaua na 'pira biriani' juu

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Moses Phiri jana alifunga bao lake la kwanza msimu huu akitokea benchi, akiiongoza Simba kushinda mabao 2-0, mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji FC, ikipigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Phiri ambaye aliumia kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza msimu uliopita dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, Desemba 21, mwaka jana, alitupia bao dakika ya 55 ambalo lilikuwa la pili kwenye mechi hiyo.

Ilikuwa ni mechi ya pili mfululizo kwa Simba kushinda baada ya Alhamisi iliyopita kuibugiza Mtibwa Sugar mabao 4-2 katika Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Hata hivyo, kama wachezaji wa Simba wangetulia wangeweza kutoka na ushindi mnono zaidi wa mabao sita kwani walikosa mengi ya wazi mbele ya kipa Danile Mgore.

Luis Miquissone peke yake alikosa mabao mawili ya wazi, Clatous Chama akikosa moja, Willy Onana, Mzamiru Yassin, Phiri na Shomari Kapombe.

Mabao mengi ambayo Simba ilikosa ilikuwa kipindi cha pili ambacho tayari Dodoma Jiji walikuwa wameruhusu bao na wameanza kupanda kushambulia ili kusaka la kusawazisha.

Kabla ya hapo ilikuwa ngumu kwa Simba kuipenya ngome ya timu hiyo ambayo wachezaji wake 10 walikuwa nyuma ya mpira, hivyo nafasi kukosekana.

Kwa mara nyingine tena, Mkongomani Jean Baleke, aliyefunga bao la kwanza katika mechi iliyopita dhidi ya Mtibwa Sugar, alipatia tena timu yake bao la kwanza dakika mbili kabla ya kwenda mapumziko lililobadilisha mifumo wa timu zote mbili kipindi cha pili.

Mpira ulianzia kwa Chama ambaye aligeuka na kumpasia Mohamed Hussein 'Tshabalala' aliyekuwa amepanda upande wa kushoto ambaye alipiga krosi iliyokoswa na mlinzi Joram Mgeveke, hivyo kumpa fursa straika huyo kuunganisha kwa


INAENDELEA UK. 20



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >